SportPesa
TZS. 433,401,140
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Serikali** yaonya mabalozi kesi ya Freeman Mbowe

UKURASA 18



**Lewandowski aomba kuondoka Bayern**

UKURASA 22

Jumamosi Agosti 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580679
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# CHADEMA wagomea mwaliko kwenda Ikulu

UKURASA 2



Aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Lushubilo Mwakabibi, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kusomewa mashtaka ya matumizi mabaya ya madaraka na ofisi. **Habari Uk. 2. PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MATAKKA, WENZAKE WAHUKUMIWA KISUTU

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu imewahukumu kifungo cha miaka...

## Serikali yapata mabilioni miamala ya simu

UKURASA 3

UKURASA WA 3

### MVUTANO WAIBUKA KORTINI KESI YA KINA SABAYA



MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imeahirisha kuendelea kusikiliza kesi ya jinai inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya...

## Msimamo wa Sumaye Katiba Mpya huu hapa



• **Ataka** mchakato uendelee, lakini... *Endelea Uk. 2*

**MICHEZO** **GOMES ATAMBA SIMBA NI MOTO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# CHADEMA yagomea mwaliko kwenda Ikulu

Na Waandishi Wetu

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimekataa mwaliko wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) uliokitaka kwenda Ikulu jijini Dar es Salaam leo kuhudhuria hafla ya k ukabidhi ripoti ya Uchaguzi Mkuu uliopita.

Mkurugenzi wa Idara ya Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alidai wamepokea mwaliko kutoka kwa Mkurugenzi wa NEC kwa ajili ya Mwenyekiti, Katibu Mkuu na aliyekuwa mgombea urais kupitia chama hicho kuhudhuria hafla hiyo.

Hata hivyo, Mrema alisema kuwa kupitia barua ya Katibu Mkuu wa CHADEMA, wamemjulisha Mkurugenzi wa NEC kuwa hawatashiriki hafla hiyo kutokana na sababu tano.

Alitaja sababu hizo kuwa zinajumuisha alichookiita ukiukwaji wa sheria na haki katika uchaguzi mkuu uliopita.

Mrema alitaja sababu ya pili kuwa ni Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, kufunguliwa kesi ya ugaidi, jambo ambalo chama hicho kinaamini ni chuki za kisiasa.

"Tunaelekeza nguvu na muda tulionao kufanya jitihada za kuhakikisha mwenyekiti wetu, viongozi na wanachama wengine waliokamatwa kwa uonevu na wanaoshikiliwa na Jeshi la Polisi wanaachiliwa huru," alisema.

Mrema aliitaja sababu ya tatu ya kutoshiriki kwao katika hafla hiyo kuwa ni madai ya kutishwa kwa aliyekuwa mgombea wao wa kiti cha urais katika uchaguzi huo, Tundu Lissu, hadi kufikia hatua ya kulazimika kukimbilia nje ya nchi.

Alidai kuwa Lissu akiwa Ubalozi wa Ujerumani, alikamatwa na Jeshi la Polisi, lakini alisaidiwa na uongozi wa ubalozi huo.

"Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, amesema hadharani kwamba Lissu hatapatiwa ulinzi wowote na polisi licha ya ukweli kwamba aliponea chupuchupu katika jaribio la mauaji la Septemba 7, 2017, jaribio ambalo halijawahi kuchunguzwa na hatua stahiki kuchukuliwa dhidi ya wahusika," alisema.

Aliitaja sababu ya nne kuwa ni NEC kutojibu barua ya Katibu Mkuu wa CHADEMA ya Novemba 25, mwaka jana yenye kumbukumbu namba C/HQ/ADM/20/TU/05/14 iliyotaka maelezo ya nani alitia saini barua na fomu za waliotangazwa kuwa wabunge wa viti maalum kupitia chama hicho na nakala ya nyaraka husika kwa ajili ya kuchukua hatua kwa kuzingatia Kamati Kuu haijawahi kufanya uteuzi wala kuwasilisha orodha ya majina NEC.

Alitaja sababu ya tano kuwa ni ajenda yao ya sasa na siku zijazo ya kuhakikisha Katiba Mpya inapatikana ili kutengeneza mfumo huru na wa kidemokrasia wa uchaguzi wa nchi.

Alidai kushiriki katika mialiko na shughuli za NEC ambayo CHADEMA wanaamini hauko huru, ni kuipa baraka za kisiasa tume hiyo na kupunguza nguvu na ari ya jitihada za kufanya mabadiliko wanayoamini yanahitajika nchini.

***Imeandaliwa na Mary Geofrey na Beatrice Inyasi (TUDARCo)**



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikagua vifaa vya maabara alipotembelea shule ya sekondari ya wasichana ya Lucas Malia, iliyopo Ruangwa, mkoani Lindi, jana. **PICHA: OWM**

# Msimamo wa Sumaye Katiba Mpya huu hapa

Na Thobias Mwanakatwe

WAZIRI Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye, ametoa msimamo wake kuhusu Katiba Mpya, akisema mchakato wa katiba inayopendekezwa uendelezwe lakini Rais apewe muda wa kujenga uchumi wa nchi kwanza.

Akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili juzi, Sumaye alisema haoni sababu kitu ambacho kinatafutwa kupambana katika suala la Katiba Mpya wakati Rais wa sasa alishakubali kulishughulikia, lakini ametaka kwanza ashughulikie kipaumbele cha kujenga uchumi.

"Tumpe Rais hiyo nafasi aliyosema, Rais yeyote katika nchi yoyote ana misingi yake ya kuweka vipaumbele vyake, na bahati nzuri hajakataa suala la katiba lakini watu wanadiriki kusema 'hata hivyo vipaumbele vyake hatuvitaki, tunataka aanze na katiba', aaah aaah sasa unawezaje kufanya hayo?" alisema.

Sumaye alisema kila Rais anapoingia madarakani kunakuwa na mambo au vipaumbele vyake, akisisitiza hata marais wote walipita walifanya hivyo.

"Ninakumbuka Hayati Rais Dk. John Magufuli alitamka kwamba katiba sio kipaumbele chake na wala hajaiahidi kwenye ilani, aliposema hivyo watu walinyamaza, hawakusema kitu na kama walisema hawakusema kwa sauti.

"Rais wa sasa amesema 'sawa Katiba Mpya nitashughulikia lakini sasa ninataka niweke kipaumbele katika uchumi'," Sumaye alisema akimkunuu Rais Samia Suluhu Hassan.

Alidai kinachofanyika sasa watu wanatafuta umaarufu wa kisiasa kwa kuwa suala la Katiba Mpya lilishughulikiwa vizuri wakati wa serikali ya awamu ya nne mpaka kufikia kwenye Bunge la Katiba na katiba iliyopendekezwa ikaandaliwa na nakala zikasambazwa.

"Tukisema tunataka Katiba Mpya, hivi tunataka tuanzie wapi? Tunataka kutupa zile hela za Watanzania ambazo ziligharamia hatua zote za Katiba Mpya? Hapana, mimi ninaamini lazima tuendelee pale ambapo tumefikia," alisema.

Sumaye alisema kama kuna marekebisho ya kufanyika kwenye katiba iliyopendekezwa, utaratibu utekelezwe ili baadaye ikifikia hatua kwenye ajenda ya katiba hiyo, watu wasianze upya.

"Kuanza kusema tena hatuitaki hiyo wakati kulikuwa na Bunge la watu 630 lililokaa miezi mitatu kujadili Katiba Mpya na fedha nyingi zikatumika, hapana.

"Watanzania tunakubali mahali tulipofikia uchumi wa nchi karibu kila kitu kilikuwa kinajifunga, biashara za watu zilikuwa zimeisha na wawekezaji walikuwa hawaji tena nchini na waliokuwapo walikuwa wavuta muda tu ili kama hakuna mabadiliko waondoke," alionya.

**CHANJO UVIKO-19**

Akizungumzia kuhusu chanjo ya UVIKO-19, Sumaye alisema hakuna sababu viongozi kupambana na kupimana vidali na vifua katika suala hilo wakati serikali ilishatangaza msimamo wake kwamba chanjo ni hiari kwa anayetaka. Alisema hakuna sababu ya kupoteza muda kupambana kati ya kundi fulani na kundi fulani kwa kuwa kufanya hivyo ni kutokujua mipaka ya kitu ambacho kiongozi anatakiwa afanye.

"Anayesema chanjo haifai sawa, kaa nyumbani kwako wewe usichanjwe, hatuwezi kuwa tunakaa tunapingana tu kwamba tunafanyeje wakati jambo hili ni la elimu kwani hakuna anayebisha kuwa ugonjwa upo, Kama ugonjwa upo, sasa tunapambanaje nao? Kuna chanjo.

## Aliyekuwa mkurugenzi Temeke mahakamani kwa tuhuma za ufisadi

Hadija Kitwana

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, Lusubilo Mwakabibi, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na mashtaka ya matumizi mabaya ya madaraka na ofisi.

Mbali na Mwakabibi, mshtakiwa mwingine ni Edward Haule ambaye alikuwa mratibu wa mradi wa DMDP.

Akisoma hati ya mashtaka jana, Wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ester Martin, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Evodia Kyaruzi, alidai kuwa washtakiwa hao kwa pamoja wanatuhumiwa katika mashtaka yote mawili.

Aliendelea kudai kuwa shtaka la kwanza la matumizi mabaya ya ofisi katika tarehe tofauti Machi, mwaka jana hadi March, mwaka huu katika maeneo ya Manispaa ya Temeke wakiwa waajiriwa kama Mkurugenzi wa manispaa na mratibu wa mradi wa DMDP wakiwa wanatelekeza majukumu yao, walielekeza ujenzi wa kituo cha basi cha Buza katika kiwanja cha Buza kinachomilikiwa na Dayosisi ya Kanisa la Aglikana bila ruhusa.

Katika shtaka la pili washtakiwa kwa matumizi mabaya ya madaraka katika mwezi na mwaka huo huo maeneo hayo wakiwa wanatelekeza majukumu yao kwa makusudi walitumia madaraka vibaya kinyume cha kifungu cha 3 kidogo (1) cha Sheria ya Ardhi.

Baada ya kumaliza kusoma mashtaka hayo Wakili Ester alida upelelezi wa shauri hilo haujakamilika na kwamba hawana pingamizi na dhamana.

Hata hivyo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu chochote, ambapo Wakili Upande wa Utetezi, Jeremia Mtobesya, aliomba mahakama kuwapa dhamana wateja wake akidai mashtaka yao hayadhaminiki.

Hakimu Kyaruzi alitoa masharti ya dhamana kuwa kila mshtakiwa anatakiwa kuwa na wadhamini wawili watakaosaini thamani ya Sh. milioni 10 pamoja na kupeleka hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo, wapewe ruhusa na hati za kusafiria wawasilishe mahakamani.

Hata hivyo, washtakiwa walishindwa kutimiza masharti na kupelekwa rumande. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 2, mwaka huu.

## Mvutano waibuka kortini kesi ya kina Ole Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imeahirisha kuendelea kusikiliza kesi ya jinai inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake baada ya mawakili wa utetezi kupinga uhalali wa wakili wa Jamhuri kumhoji shahidi wa pili wa utetezi Silvester Nyegu (26) kupitia maelezo aliyoandika awali kituo cha polisi.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, shahidi huyo wa utetezi alidai mahakamani huko kwamba hakuwahi kuandika maelezo yoyote kituo cha polisi, wala kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Vilevile, shahidi huyo alidai kwamba anafahamu kuwa endapo mahakama hiyo itamtia hatiani kifungo chake kitakuwa cha maisha au miaka 30. Wakili Kweka aliiomba mahakama hiyo kutumia kifungu namba 154 cha Sheria ya Ushahidi kutumia maelekezo ya shahidi aliyoandika kituo cha polisi kumhoji.

Wakili huyo alidai kwamba kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria, maelezo hayo yanaweza kuwa ya shahidi au kumhusu mwenyewe, pia sio lazima maelezo yawe yameandikwa na shahidi na wakati mwingine sio lazima aonyeshwe maelezo hayo mahakamani kwa kuwa ni matakwa ya kisheria.

"Tunachokifanya hapa kimekidhi kigezo cha kifungu cha Sheria ya Ushahidi Na. 154, na katika muktadha huo kwa kuokoa muda wa mahakama, tunaomba ombi la utetezi litupiliwe mbali na turuhusiwe kuendelea kumhoji shahidi huyu," alidai Wakili Kweka.

Wakili wa Utetezi, Edmund Ngemela, alipinga vikali maelezo hayo yanayodaiwa ni ya shahidi huyo kutumika kumhoji kwa kuwa sheria imeelekeza, ili kumuuliza maswali shahidi, maelezo yanatakiwa kuwa yameandikwa na muhusika mwenyewe.

"Shahidi ameieleza mahakama kwamba maelezo hayo hayafahamu na hakuwahi kuhojiwa popote, hivyo tunaomba mahakama kukataa jambo hilo na kielelezo chenyewe siyo kwa sababu hakijapokelewa mahakamani na hauwezi kumhoji shahidi wakati kielelezo hicho hakijapokelewa kisheria," alidai.

Wakili mwingine wa Utetezi, Silvester Kahunduka, alidai mahakamani huko kuwa kifungu cha sheria ya ushahidi namba 154 kilichotumiwa na wakili wa serikali hakikufuata takwa la kisheria.

"Wakili anasema shahidi aliwahi kuandika maelezo polisi wakati shahidi anadai kwamba, hakuwahi kuandika maelezo sehemu yoyote na tunatumaini kwamba mteja wetu hatatendewa haki, maelezo hayo yasitumike kumhoji maswali kwa kuwa hayafahamu," alidai.

Baada ya mvutano huo wa kisheria, Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Odira Amworo, aliahirisha kesi kwa dakika 15 kwenda kupitia hoja za mawakili hao.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio katika makato ya makusanyo ya miamala ya simu. **PICHA: JUMENNE JUMA**

# Serikali yapata mabilioni tozo za miamala ya simu

**Na Romana Mallya**

WAKATI wananchi wakiendelea kulia na makato yatokanayo na tozo ya miamala ya simu, serikali imesema ndani ya wiki nne tangu yaanze imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 48, huku ikiwaomba waendelee kuvumilia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu tozo za miamala ya simu, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema siku siyo nyingi watatoa tamko.

Alisema tamko hilo litahusiana na mfumo upi nzuri unaohusisha namba ambazo zimeangaliwa kwa kuhusisha upande wa serikali na watoa huduma.

"Hapa katikati yametokea maneno mengi ambayo ni vizuri tuyaweke sawa, yapo maeneo ambayo hili jambo limeathiri sana sekta kwa maana kwamba shughuli za kimiamala umeshuka sana wengine wakielezea kuwa wameacha kufanya hivyo.

"Watanzania wameendelea kufanya shughuli za miamala na wametoa sauti zao ili hili jambo lifanyike kwa ufanisi zaidi ni vizuri wakaliangalia, hili linaendelea kufanyika na namba zinacheza mle mle.

Waziri Nchemba alisema kabla hawajaanza tozo hizo, kulikuwa na miamala milioni tisa na milioni 10 na sasa inacheza humo humo.

"Katika wiki nne tangu tumeanza hii shughuli wakati tukisubiri marekebisho ambayo tunapanga kuyafanya, shughuli hii ya utozaji tozo kwenye miamala ilianza Julai 15, mwaka huu mpaka tunaongea leo (jana), ukioanisha na mapendekezo tuliyopangilia, tumekusanya bilioni 48.489," alisema.

Alisema kwa wiki mbili zilizopita tayari wameshapeleka zaidi ya Sh. bilioni 22 kwenye maeneo ambayo hawana vituo vya afya ambapo kwa hesabu ya haraka vitajengwa zaidi ya 90.

"Leo (jana) zaidi ya Sh. bilioni 15 zimetolewa ili kwenda kwenye eneo hilo ambapo itafanya kwa sasa jumla ya vituo vya afya zaidi 150 kwenye maeneo haya kuwahi kuwa na kituo.

Zaidi ya Sh. bilioni 7 ni kwa ajili ya madarasa ili kujiandaa kupokea watoto wa kidato cha kwanza mwakani," alisema.

Waziri Nchemba alisema kwenye sheria hiyo walipoitunga ilikuwa inatumika pande mbili Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar, ambapo ndani ya wiki nne wamekusanya Sh. bilioni 1.66.

"Miezi hii minne eneo hili lina matokeo, watu wachukue hivyo hivyo, hii nchi ni yako, fedha ni yako na hii iliyokusanywa ni yako, hivi vituo 150 vinaokoa maisha ya watu wako na madarasa haya zaidi ya 500 ni watoto wako.

"Na utaratibu tuendeshe vipi vizuri ni wetu sote tumepokea sana hayo, tumepokea maelekezo na tutafanyia kazi watu wasiwe na mashaka serikali ni sikivu imepokea maelekezo

Katika utaratibu wa kawaida mtaona malengo hayaathiriki na shughuli zimeendelea vizuri, miamala milioni 9.9. milioni 10 na milioni 10.0 ni jumlisha na kutoa.

Alisema wizara inaamini na inatarajia wanakokwenda kasi ya utumiaji fedha itaongezeka kwa sababu kutumiana inategemeana na ile unayoishika kwenye mkono ambayo ipo tayari kwenye matumizi.

Pia alisema watakapopeleka zaidi ya Sh. bilioni 48 kwenye uchumi huku wakiendelea na uratibu wa ulipaji wa madeni wa makandarasi na watoa huduma, mbeleni wanalenga kuweka zaidi ya Sh. bilioni 600.

Alisema kwa ujumla wanapanga kuweka zaidi ya trilioni 3 ambazo wanaamini kasi ya fedha ya kubadili mikono itakuwa kubwa na watu watatumiana miamala zaidi.

Kuhusu matokeo ya kamati iliyoundwa kuhusiana na tozo za miamala ambayo baadae ilitakiwa kwenda kufanya kazi zaidi waziri huyo alisema kabla ya mwisho wa mwezi huu, Waziri Mkuu atakuwa ameshaipokea taarifa hiyo na ikiwezekana uamuzi utolewe kwa ajili ya kile kitakachofanyika.

"Kilichokawiza ni namba, zilipotoka zilivyokuwa zinasomeka, wakati tumeziweka tulizikadiria kama namba zenyewe lakini pembeni tulizikadiria kama watoa huduma wana wanazipata kuanzia hapo.

"Lakini jumla anayoipata mwananchi inakuwa ni jumla ya gharama za mtoa huduma na gharama ilizoweka serikali, katika hali ya kawaida tukawa tunaangalia, mfano eneo la watumiaji serikali inachukua Sh. 10, kutoka 1000 kwenda 2000 mtoa huduma anachukua 360," alisema.

Alisema kwenye hilo wakasema wawaombe wananchi wawe wavumilivu wajipe muda wa kushirikisha wenzao (watoa huduma) kuangalia walivyojumlisha mzigo umekuwa mkubwa wa wananchi, hawawezi kuangalia nani apunguze wapi.


SPYTECH Security Supplies ltd

SPYTECH AUCTION MART & COURT BROKERS

NIC LIFE HOUSE BUILDING, SOKOINE DRIVE ROAD THIRD FLOOR, P.O.BOX 75602 DAR ES SALAAM
MAFINGA P.O.BOX 480 / MOB: +255 755 815 974 / +255 658 815 974
MBARALI MBEYA P.O.BOX 46

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 21/08/2021**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MUCOBA BANK PLC-MAFINGA** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA MUCOBA BANK PLC-MAFINGA. MNADA UTAFANYIKA KUANZIA TAREHE **22/09/2021** SIKU YA JUMATANO NA KUENDELEA KUANZIA **SAA 4:00 ASUBUHI MPAKA 12:30 JIONI** MAHALI ZILIPO DHAMANA ZA WADAIWA. ORODHA YA WADAIWA NI KAMA WAFUATAO:

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALA ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|
| WITNESS D. CHUMI | NYUMBA | MAFINGA-KINYANAMBO |
| JAPHET L. MLEMBE | NYUMBA | MUFINDI-IGOWOLE |
| NEEMA R. MGAYA | NYUMBA | MUFINDI-IGOWOLE |
| THOMAS Y. KIDENYA | NYUMBA | MAFINGA-KINYANAMBO "A" |
| HELIETH J. KALINGA | NYUMBA | MAFINGA-IHONGOLE |
| SHABAN THABIT MSOLA | NYUMBA | MAFINGA-CHANGARAWE-IGAWA |

**NB: MASHARTI YA MNADA**

MNUNUZI ATAKAE BAHATIKA ATATAKIWA KULIPA 25% YA BEI ILIYOFIKIWA PAPO HAPO. NA KIASI KILICHOBAKI KILIPWE NDANI YA SIKU 14, KINYUME NA HAPO PESA ILIYOTOLEWA AWALI HAITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA TENA. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI MILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE NA GHARAMA ZA KWENDA KUANGALIA/KUKAGUA NYUMBA SHAMBA/VIWANJA NI ZA MTEJA MWENYWE. IKUMBUKWE KUWA MDHAMINI NI SEHEMU YA MKOPAJI. LIPA DENI LAKO KABLA YA 22/09/2021 UKISUBIRI MPAKA SIKU YA MNADA GHARAMA ZITAONGEZEKA TSHS 100,000/= WASILIANA NASI **KWA NAMBA 0755815974/0623815974.**

**WOTE MNAKARIBISHWA**

*E-MAIL:spytechtz@gmail.com*

21648002

# Matakka na wenzake wahukumiwa

**Na Hadija Kitwana**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewahukumu kifungo cha miaka mitano jela au faini ya Sh. milioni 10 katika kesi ya matumizi mabaya ya madaraka iliyokuwa ikimkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), David Mattaka na wenzake wawili.

Aidha katika shtaka la tatu la kuisababishia hasara Serikali Dola la Marekani 42,459,316.12 linalowakabili Mattaka ameachiwa huru, kutokana na upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha kosa hilo.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janet Mtega, alisema kuwa washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita ambapo shtaka la kwanza hadi la tano linamkabili mshtakiwa wakwanza Mattaka.

Aliendelea kusema kuwa katika mashtaka yanayomkabili Mattaka ni matumizi mabaya ya madaraka, matumizi mabaya ya ofisi na kuisababishia hasara Serikali zaidi ya Sh. bilioni 71.

Katika shtaka la sita la kughushi linawakabili mshitakiwa wa pili na watatu ambao aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Dk. Ramadhan Mlinga na aliyekuwa mwanasheria wa mamlaka hiyo, Bertha Soka.

Aliendelea kusema kuwa ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri umethibitisha bila kuacha shaka yoyote katika shtaka la kwanza, la pili, la nne na la tano yanayomkabili Mattaka na amemhukumu kulipa faini ya Sh. milioni mbili au kifungo cha mwaka mmoja jela kwa kila kosa.

Katika shtaka la tatu la kuisababishia hasara serikali linalomkabili Mattaka upande wa Jamhuri imeshindwa kuthibitisha kutokana na kielelezo kilichopelekwa mahakamani ambacho ni nyaraka inayoonyesha kiwango cha fedha inayodaiwa kusababisha hasara kwa serikali tofauti na kiwango cha fedha kilichoandikwa katika hati ya mashtaka, hivyoshtaka hilo amemuachia huru.

Aliendelea kusema kuwa katika shitaka la sita la kughushi linalowakabili Mlinga na Bertha wametiwa hatiani, baada ya upande wa Jamhuri kuthibitisha bila kuacha shaka yoyote ambapo aliwahukumu kulipa faini ya Sh. milioni mbili kwa kila mmoja au kifungo cha mwaka mmoja jela.

Kabla ya kusoma kwa hukumu hiyo Wakili wa Serikali kutoka TAKUKURU, Joseph Kiula, aliitaka mahakama itoe adhabu kali ili liwe fundisho, kwani mshtakiwa wa kwanza ambaye ni Mattaka hiyo ni kesi ya pili kutiwa hatiani na kuhukumiwa kulipa faini au kifungo jela katika kesi ya uhujumu uchumi namba 277/2017 ya matumizi mabaya ya madaraka, kula njama na kuisababishia Hasara Serikali iliyokuwa kwa Hakimu Victoria Nongwa.

Hata hivyo, wakili Kilua ameeleza kuwa hana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washtakiwa Mlinga na Bertha.

Akijitetea baada ya kutiwa hatiani ili asipewe adhabu kali, Mattaka aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwani yeye ni mtu mzima sana wa miaka 70, pia anasumbuliwa na tezi dume, shinikizo la juu la damu na sasa anapata magonjwa mengine.

Hata hivyo, washtakiwa hao walilipa faini na kuachiwa huru




Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Edward Mbanga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Tiba ya Asili ya Mwafrika, yanayotarajiwa kufanyika Kitaifa Agosti 28-31, mwaka huu katika jiji hilo. Kushoto ni Mkurungenzi wa Idara ya Tiba wa wizara hiyo, Dk. Caroline Mayengo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bunge laitahadharisha serikali madeni ya TPDC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeitahadharisha serikali kuwa inaliua Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) kutokana na kutolipa madeni inayodaiwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alisema Shirika hili linashindwa kufanya kazi kutokana na kudai fedha nyingi kwa Shirika la Umeme nchini(TANESCO) zaidi ya Sh. bilioni 421.

"TPDC walikubaliana na TANESCO kila wiki ilipwe Sh.Bilioni tisa lakini sasa hivi TANESCO wakakaa inaweza kufika hata mwezi hawajalipa hata senti tano," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kamati hiyo imeitaka TANESCO kuheshimu mkataba wao na TPDC wa kulipa fedha hizo.

Aidha, alisema kuna deni benki ya EXIM ambalo serikali wanalipa lakini wamewawekea TPDC kama ni deni lao na kuonekana shirika linafanya kazi kwa hasara.

"Matokeo ya hili deni TPDC hawawezi kukopa hata fedha benki kufanya kazi, au kuingia ubia kwa kuwa wanaonekana wana negative balance kwa hiyo PAC imeagiza TANESCO walipe hizo fedha na serikali ichukue deni la EXIM ili lifutwe kwenye vitabu na TPDC isiwe na deni na kufanya biashara," alisema.

Alisema PAC imeshauri serikali ichukue deni hilo na kuliweka kama mtaji kwa TPDC ili ifanye kazi kwa ufanisi.

"TPDC ndio wanahangaika na bomba la mafuta la kutoka Hoima, sasa watafanyaje biashara kama hawana fedha, kwa hiyo serikali inaliua shirika kwa mikono yake yenyewe, kwasababu tunajua serikali hailipi TANESCO na mashirika mengi hayalipi na matokeo yake inashindwa kulipa TPDC," alisema.

Alisema TPDC ni shirika kubwa ambalo lingeleta uchumi mkubwa kwa taifa kwa kusambaza gesi.

"Kwa sasa wakiambiwa wasambaze gesi wanasambaza na nini?, kama REA(Wakala wa Umeme Vijijini) wanapewa fedha na serikali kusambaza umeme vijijini na RUWASA (Wakala wa Maji Vijijini) wanapewa fedha ya kusambaza maji, kwanini TPDC wasipewe fedha na serikali kusambaza gesi?,"alisema.

Kufuatia deni hilo, alisema kamati imeitaka Wizara ya Nishati na Ofisi ya Msajili Hazina kuangalia namna ya kubadili Sheria ya Mfuko wa Gesi na Mafuta ambayo inafanya TPDC kuwa na shida ya ukwasi.

## Serikali yahimiza upigaji wa 'nyungu'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI chanjo ya corona ikiendelea nchini, serikali imewahimiza wananchi kutoacha matumizi ya 'nyungu' kujifukiza pamoja na dawa asili zilizosajiliwa.

Kaimu katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto, Edward Mbanga, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya tiba asili ya Mwafrika.

Mbanga, alisema wakati huu ambapo chanjo ya corona inaendelea kutolewa, anaikumbusha jamii kutoacha kutumia nyungu, dawa za asili zilizosajiliwa na kuzingatia maelekezo kutoka kwa wataalamu.

"Pia msiache kuchukua tahadhari muhimu za kujikinga na ugonjwa huu kwa kila mmoja kuvaa barakoa kwa usahihi, kuepuka misongamano, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vipukusi na kukaa umbali wa mita moja na kumuomba mungu," alisisitiza Mbanga.

Aidha, alisema serikali inaendelea na urasimishaji wa tiba asili wenye lengo la kuboresha tiba asili nchini.

"Kupitia urasimishaji huu dawa nyingi za tiba asili zikiboreshwa zinaweza kutumika kwa wingi kutibu magonjwa mbalimbali na hata kuuzwa nje ya nchi kama nchi nyingine zinavyofanya," alisema Mbanga.

Akizungumzia maadhimisho ya siku ya tiba ya Mwafrika, alisema lengo lake ni kuhamasisha uendelezaji na uboreshaji wa tiba asili katika nchi za kiafrika.

"Mwaka 2021 ni mwaka wa 19, tangu maadhimisho haya yalipoanza kuadhimishwa mwaka 2003 ambapo mwaka huu kaulimbiu ni 'mchango wa tiba asili katika kukabiliana na UVIKO-19 kanda ya Afrika,'" alisema.

Alifafanua kuwa kaulimbiu hiyo inakumbusha jinsi dawa za asili zinavyosaidia katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona na magonjwa mengine.

Kadhalika alisema katika kupambana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambaukiza, wananchi wanahimizwa kuhifadhi mitidawa ambayo ndiyo chachu ya tiba asili.

"Wilaya zote nchini zishirikiane na waganga wenyewe katika kutenga maeneo yenye mitidawa na kuhifadhi," alisema.

Vilevile, aliwataka waganga wa tiba asili wote nchini kupeleka dawa zao kupimwa katika maabara ya Mkemia mkuu wa serikali ili zithibitishwe kuwa zina usalama.

**TANGAZO**

# Tukutane sheli

# BASHIRI KATIKA EPL ILI KUSHINDA TOYOTA RAV4




betPawa inatoa nafasi kwa wateja wote kuanza msimu mpya wa Ligi kuu ya Uingereza wakiwa na gari mpya.

Mtanzania mmoja atabahatika kujishindia Toyota RAV4 mpya kabisa. Watano watajishindia PS5 na CD ya Fifa 21, na wawili watapata shilingi laki 5 kila mmoja kwa ajili ya shopping Shoppers supermarket.

Tumia nafasi yako kushinda kikubwa ZAIDI, bashiri mechi yoyote ya ligi kuu Uingereza kupitia betPawa na uingie katika droo.

Una nafasi hadi Jumapili ya tarehe 29 Agosti kushiriki na washindi 8 watapatikana katika droo siku ya Jumatatu tarehe 30 Agosti.

Wataalikwa Dar es Salaam katika shindano la upigaji penalti mwezi Septemba.
Mshindi ataondoka na Toyota RAV4, na hakuna mtu ataondoka bila zawadi.

Je utakua mshindi? Unaweza kushiriki kwa kubashiri kwa kiwango kidogo cha TSH 1 tu.

Tukutane sheli na betPawa!
Ingia **betpawa.co.tz/epl-launch-giveaway**

**betPawa**

Cheza kiasi. 18+. betPawa imesajiliwa chini ya bodi ya michezo ya kubashiri ya Tanzania. Leseni #SBI000000026.

216418102

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Weledi upewe nafasi kuelekea msimu mpya

**LIGI** Kuu Tanzania Bara msimu mpya wa 2021/22 inatarajia kufanyika kuanzia Septemba 29, mwaka huu kwa kushirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Timu hizo zitakazowania ufalme huo ni pamoja na mabingwa Simba, Yanga, Azam FC, Biashara United, KMC FC, Polisi Tanzania, Kagera Sugar, Mtibwa Sugar, Dodoma Jiji FC, Tanzania Prisons, Coastal Union, Ruvu Shooting, Geita Gold FC na Mbeya Kwanza.

Mbali na ligi hiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kuanza maandalizi kuelekea msimu mpya, pia Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), First League (zamani Ligi Daraja la Pili), Ligi Kuu ya Wanawake na Ligi Daraja la Kwanza Wanawake yanaendelea kwa wakati mmoja.

Maandalizi sahihi kwa timu zote zinazoshiriki ligi hiyo ndiyo yatakayozalisha matokeo mazuri na hatimaye mwisho wa msimu kupata bingwa anayestahili na si vinginevyo.

Kwa sasa kila timu inaendelea kupiga hesabu zake vyema kwa kuanzia kwenye mchakato wa usajili, kuboresha benchi la ufundi sambamba na kutekeleza programu sahihi ya kambi kwa sababu inafahamika ushindani utaongezeka kutokana na dau nono la zawadi lililotangazwa na wadhamini, Kampuni ya Azam Media.

Lakini hesabu hizo zinaweka kukamilika au kuonekana zimetendewa haki kama kila mmoja kwenye timu hizi akatekeleza majukumu yake ipasavyo, bila shinikizo kutoka upande mwingine. Inaweza kuonekana suala la weledi linatakiwa kutekeleza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara pekee, lakini si kweli, weledi huu unatakiwa uonekane kwa vitendo hadi kwenye Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi zote za wanawake, kwa sababu tunahitaji kufikia mafanikio.

Nipashe inajua timu zote sasa zimetolewa macho katika suala la usajili, lakini ikumbukwe mchakato huu utaonekana wenye mafanikio kama utafanyika kwa kufuata mapendekezo ya makocha na si kwa misingi ya kukomoana baina ya klabu moja na nyingine. Tumeshuhudia hivi karibuni timu moja ya Ligi Daraja la Kwanza ikisajili wachezaji nyota waliowahi kutamba katika klabu kongwe na Taifa Stars, lakini hili litaonekana lenye uzito kama wamiliki na wasimamizi wake watatekeleza mipango yao ya msimu ujao kwa weledi.

Jambo la msingi ni kuona wamiliki wa timu wanawaachia makocha na wakurugenzi wa ufundi nafasi ya usajili na sio kuacha watu waingilie uamuzi wao, ili baadaye mambo yatakayokwenda vizuri wapongezwe au yatakapoharibika wawajibike kutokana na kile walichokipanda.

Tuwakemee viongozi ambao wanasimama kama makocha kwa sasa lakini pia wanasajili wachezaji ambao wanafahamu wazi kwamba hawatapata nafasi ya kucheza na baadaye kupelekea vipaji vyao kupotea. Kinachohitajika ni kutumia ripoti ya mwalimu katika kufanya usajili na hii itasaidia msimu ujao kuwa na ushindani wa kweli na kila timu kuwa sawa kwa ajili ya kusaka ushindi.


Muhimu kwa sasa ni kuhakikisha timu zote zinafanya maandalizi mazuri na kufanya kila kitu kionekane kimetekelezwa kwa utaratibu uliopangwa kwa sababu kwa kufanya hivyo itasaidia nchi kuwa na ligi bora na yenye mvuto, lakini ikimpa nafasi nzuri Kocha wa Stars, Kim Poulsen kuteua wachezaji kwa ajili ya kushiriki mashindano mbalimbali yaliyoko mbele yetu.

Lakini, weledi huu pia unatakiwa uwepo na kwa waamuzi ambao mwisho wa siku wanapewa dhamana ya kuchezesha mechi ambazo bingwa hupatikana. Hapa ndio uadilifu wa kiwango cha juu unahitajika ili kutoionea timu yoyote.

Kila timu inatakiwa kujipanga kuvuna pointi za kutosha katika mzunguko wa kwanza na kujiondoa kwenye presha ya kupambana kujinusuri kushuka daraja wakati msimu unapoelekea lala salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Gonga gogo usikilize mlio wake

Na Barnabas Maro

**NI** vizuri kuligotagota (gongagonga) pande la mti ukausikia mlio linaotoa, methali hii inatufunza umuhimu wa kufanya uchunguzi wa kufaa kabla ya kujitoa au kuanza jambo fulani. Kwa njia hii huwa tumejiandaa vya kutosha kupambana na litakalotokea.

Toleo lililopita nilieleza umuhimu na faida ya kuwa na wachezaji wachache kutoka nje ya Tanzania ili nyota wetu wapate nafasi kusajiliwa na timu kama wakipewa nafasi hizo.

Wahenga walisema "Mwanzo kokochi, mwisho nazi." Kokochi ni tumba dogo linaloishia kuwa nazi. 'Tumba' ni ua ambalo halijachanua; fumbo. Kwa hiyo mwanzo wa nazi ni ua au tumba. Methali yatukumbusha kwamba kila jambo huwa na mwanzo wake. Hata jambo likawa kubwa vipi, mwanzo wake huwa mdogo.

Kwa kuwa hata watoto huanza kutembea dede, kabla ya kutembea sawasawa ndivyo walivyo wanamichezo wote. Wachezaji kandanda wengi wageni wanaosajiliwa na timu zetu, zaidi Yanga na Simba, walifundishwa kwao kabla ya kuajiriwa na vilabu vya nchi za nje.

Ilivyo sasa, Tanzania imekuwa kimbilio la wachezaji wanaotoka nje ya nchi yetu kwani wanalipwa fedha zaidi ya wanazolipwa kwao ilhali wachezaji wa Tanzania hulipwa fedha kiduchu.

Ni dhahiri kuwa fedha wanazolipwa wachezaji kutoka nje ya Tanzania huwanufaisha wao na nchi zao ilhali wachezaji wetu hulipwa fedha (-enye kuwa na kiwango cha chini cha udogo)

Si hilo tu kwani fedha zetu huzinufaisha nchi watokazo wachezaji wa nje. Maana yake fedha hizo hubadilishwa kwa thamani ya nchi zao kama ni za Uingereza, Ufaransa, Ureno n.k. Ni nchi zilizokuwa chini ya himaya ya nchi hizo kabla ya kuwa huru.

Swali rahisi la kujiuliza ni hili: Kama wachezaji wa kigeni ni mahiri kwa uchezaji wa kandanda mbona hawaendi nchi nilizotaja ambazo wachezaji hulipwa fedha nyingi maradufu ya wanazolipwa makwao na hapa Tanzania?

**Huondoshwa bila kulipwa stahiki zilizokubaliwa na pande zote yaani waajiri na waajiriwa! Malalamiko yao hufikishwa katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na inaposhindikana hupelekwa FIFA ambako timu husika hulazimishwa kuwalipa wadai. Fedheha iliyoje?**

Kwa mtindo huo, tazama hasara tupatazo; wakati tunawalipa wachezaji wa ughaibuni fedha nyingi, wachezaji wetu kindakindaki (halisi) hulipwa kiduchu ikilinganishwa na mishahara wanaolipwa wachezaji kutoka nje ya Tanzania.

Kinachoshangaza zaidi ni Tanzania kuwa na wachezaji wengi mahiri wa kabumbu kuliko hao wanaopatikiwa na kulipwa fedha nyingi kuliko wenyeji! Pamoja na 'umahiri' wa wachezaji wa ughaibuni lakini baadhi yao huachwa hata kabla ya kumaliza muda wa mikataba yao kwa kutokidhi haja!

Huondoshwa bila kulipwa stahiki zilizokubaliwa na pande zote yaani waajiri na waajiriwa! Malalamiko yao hufikishwa katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na inaposhindikana hupelekwa FIFA ambako timu husika hulazimishwa kuwalipa wadai. Fedheha iliyoje?

Husemwa "Mgala muuwe na haki yape mpe." Maana yake mlaumu mgala inapobidi lakini mpe sifa anayostahiki. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa inafaa kuwalaumu watu kutokana na udhaifu wao lakini tuwasifu wanapostahiki.

Vilevile "Mbio za kasa si mbio lakini humfikisha aendako." Kasa ni mnyama wa baharini anayefanana na kobe. Maana ya methali hii ni kwamba kasa hana mbio bali huenda taratibu na mwendo wake kumfikisha aendako. Huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu mnyonge au asiyekuwa na uwezo fulani lakini anayeendelea kujitahidi na hatimaye hufanikiwa.

Hii ni methali ya kumtia mtu shime ili afanye jambo analokabiliwa nalo hata kama litamchukua muda mrefu. Kwa maana nyingine, "Mungu humsaidia mtu anayejisaidia." Hapa twafunzwa umuhimu wa kujitahidi kufanya jambo badala ya kulalamika tu au kungoja Mungu atusaidie!

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

**HABARI KITAIFA**

# Kampeni ya usafi GIZ yairidhisha serikali

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imepongeza kampeni ya usafi inayotekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani GIZ kupitia mradi wake wa DeveloPPP ambapo limepanga kuwafikia watu 25,000 kwenye Mkoa wa Dar es Salaam.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Wilaya ya Temeke, Ally Hatibu, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya usafi ni afya katika wilaya hiyo kwenye hafla iliyofanyika Mbagala. inayotekelezwa na Shirika la Emmanuel Borotherhood Foundation (EBF) na BINGWA Laboratories.

Hatibu aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema kampeni hiyo ina lengo la kudhibiti magonjwa yatokanayo na uchafu kwa mama na baba lishe, makondakta na madereva wao na madereva wa bajaji italeta manufaa makubwa kwa jamii.

Mradi wa usafi ni afya unaofadhiliwa na Wizara ya Maendeleo ya Ushirikiano wa Kiuchumi ya Ujerumani unatekelezwa na GIZ kupitia mradi wake wa Developpp. Hatibu alisema Wilaya hiyo ina changamoto mbalimbali za magonjwa yatokanayo na uchafu, ingawa serikali imesogeza huduma za afya karibu na wananchi na kuboresha upatikanaji wa dawa bado magonjwa hayo yanagharimu fedha nyingi kwa serikali na familia.

Alisema kampeni hiyo italeta ufumbuzi wa changamoto hizo kwani mbali ya kutoa elimu ya usafi walengwa watapewa bidhaa mbalimbali za usafi ikiwemo sabuni za kunawa mikono, vitakasa mikono, dawa za kuulia vijidudu vya magonjwa ya kuambukiza.

"Ninawapongeza sana kwa kuendesha mradi huo na napenda kuwahakikishia kuwa serikali ya awamu ya sita itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kama ilivyo kwa GIZ kuwawezesha wananchi kujikwamua katika changamoto za afya," alisema

Msemaji wa GIZ, Lesue Stephen, alisema shirika hilo linaungana na serikali na wadau wengine kuhamasisha jamii kupitia kampeni ya usafi ni afya ili kuchochea mabadiliko ya tabia chanya ya kujijali kimwili na usafi wa maeneo ya kazi na mazingira ya nayotuzunguka.




Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Ally Hatibu (wa pili kushoto), akigawa bidhaa kwa mamalishe zitakazotumika katika kampeni ya usafi ni afya inayoendeshwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kupitia mradi wake wa DeveloPPP, iliyozinduliwa wilayani humo, mkoani Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mwakilishi wa Balozi wa Ujerumani, Johannes Sperrfechter **PICHA: MIRAJI MSALA**

# PM aupa mgodi wa dhahabu masharti

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameutaka uongozi wa mgodi wa dhahabu wa Namungo kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri yatakayowawezesha wachimbaji wadogo kunufaika.

Pia, Waziri Mkuu ameagiza mmiliki wa mgodi huo, afike Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma Septemba 10, 2021 akaeleze mipango yake ya kuendeleza mgodi huo pamoja na wachimbaji wadogo.

Alitoa maagizo hayo jana alipotembelea mgodi huo uliopo wilayani Ruangwa, Lindi akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua shughuli za maendeleo.

Waziri Mkuu alisema uongozi wa mgodi huo umeingia mikataba na wachimbaji wadogo hivyo amewataka waweke mazingira mazuri yatakayowawezesha wachimbaji hao kunufaika.

"Lazima kuwe na mikataba ambayo pia inawapa fursa wachimbaji wagodo kuchimba na kujipatia kipato na haya ndiyo malengo ya nchi. Rasilimali hizi ni za Watanzania wote."

Alisema serikali ina wajibu wa kusimamia mikataba kati ya wachimbaji wadogo na mwenye mgodi na iwapo mikataba hiyo haitekelezwi vizuri italazimika kuangalia upya leseni hiyo.

"Fanyeni shughuli zenu kwa kuzingatia mikataba halali inayozingatia sheria za nchi. Jipangeni vizuri kwa sababu serikali itaendelea kusimamia haki zenu ikiwa ni pamoja na mikataba."

Waziri Mkuu alisema eneo hilo ni muhimu kwa sababu mbali na serikali kunufaika kwa kukusanya mapato pia wananchi wengi wamepata ajira katika mgodi huo.

Akizungumza na wananchi katika eneo linalotarajiwa kujengwa mgodi wa graphite katika kijiji cha Matambarare, Waziri Mkuu aliwataka wachangamkie fursa ya uwepo wa mgodi huo.

Naye, Naibu Waziri wa Nishati Prof. Shukuru Manya, alisema Serikali imeweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali ya madini iliyoko nchini.

Amesema mkoa wa Lindi ikiwemo wilaya ya Ruangwa kuna utajiri mkubwa wa madini ya aina mbalimbali. "Namungo kuna leseni nne za uchimbaji wa kati lakini imetoa nafasi kwa wachimbaji wadogo 500."

Kwa upande wake, Meneja wa Kampuni Lindi Jumbo inayochimba madini ya graphite, Paul Shauri, alisema mgodi huo utaanza kuzalisha ifikapo Agosti, 2022.

Alisema sehemu ya fedha za ujenzi wa mradi huo wamekopa kutoka benki ya CRDB na kwamba wamepanga kuanza kulipa deni hilo la Sh. bilioni 46 baada ya kuza madini hayo.

# Bil. 84/- za Canada zaboresha mafunzo ya walimu

**Na Faustine Feliciane**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi imesema fedha za ufadhili Sh. bilioni 84 kutoka Serikali ya Canada zitasaidia kuboresha mafunzo ya elimu kwa walimu na kuboresha miundombinu kwenye vyuo vya serikali.

Kauli hiyo imetolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Leonard Akwilapo, alipokuwa akizungumza katika mkutano uliokutanisha wadau mbalimbali kujadili na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi wa kuboresha mafunzo ya ualimu nchini ambao unafadhiliwa na Serikali ya Canada.

Serikali ya Canada imetoa fedha hizo kwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara hiyo.

Mradi huo wa miaka mitano umefanyika kwa miaka mitatu sasa na unatarajiwa kukamilika baada ya miaka miwili.

Amesema walimu wakifundishwa katika mazingira mazuri itasaidia kwa kiasi kikubwa kupata walimu bora na wenye kukidhi mahitaji ya sasa.

Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano.

" Mradi huu umelenga zaidi kuimarisha ufundishaji kwa ujumla wake katika vyuo vya uwalimu sambamba na kutengeneza miundombinu ya vyuo 35 vya serikali na kufanyiwa maboresho mbalimbali kulingana na mahitaji katika kila chuo "alisema Akwilapo

Alisema mradi huo pia kwa kiasi kikubwa umelenga kuboresha eneo la mafunzo kwa walimu pamoja na kuboresha miundombinu.

"Kupitia mradi huo vipo vyuo ambavyo vimejengewa maktaba sita ambavyo ni pamoja na chuo cha Tukuyu, Dakawa, Morogoro, Butimba , Mpwampwa pamoja na Kasulu, mradi huu utaimarisha kwa kiasi kikubwa eneo la mafunzo," alisema Akwilapo.

Aidha amesema mbali na ukarabati pia mradi huo unatoa Mafunzo kwa wakufuzi kazini na kutoa vifaa vya kufundishia vya TEHAMA.

"Mafanikio ya mradi huu ni makubwa sana kwani mpaka sasa tumefanikiwa kujenga chuo kipya cha Kabanga ambao muda sio mrefu kinakwenda kuzinduliwa, hakika tunaishukuru Serikali ya Canada kwa ufadhili wa mradi huu," aliongeza.

Alibainisha kuwa mradi huo ambao umeshaanza miaka mitatu iliyopita utakamilika baada ya miaka miwili ambapo baada ya kukamilika, serikali inatarajia kutoa walimu wenye sifa zinazotakiwa na stadi bora za kufundishia.

Mwakilishi Serikali ya Canada, Hellen Fytche, alisema Canada itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuleta miradi mbalimbali yenye kuleta maendeleo chanya.

Aidha alitoa wito Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na utawala wa maendeleo na vyuo vya uwalimu kufikiria miradi mingine kama huo yenye kuleta tija kwa miaka ijayo.

# Sababu kuvurugika ratiba ndege ATCL

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Ndege Tanzania (ATCL) imesema matengenezo ya ndege yanayoendelea kufanyika, yamesababisha ratiba ya safari zake kuvurugika kwa kipindi cha wiki mbili.

Imesema matengenezo hayo yamesababisha baadhi ya safari kuahirishwa na inawaomba radhi wateja wake.

Akiwasilisha taarifa ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Albinus Manumbu, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa kampuni hiyo, Josephat Kagirwa, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema matengenezo yanafanyika kwa sababu wanajali usalama wa abiria pamoja na wafanyakazi wa kampuni hiyo.

“Kampuni itahakikisha matengenezo hayo ya ndege yanamalizika kwa wakati yakitokea mabadiliko yoyote ya safari, ATCL hutoa taaarifa kwa abiria wanaotarajiwa kusafiri kabla ya safari au hata baada ya kufika uwanjani,” alisema.

Alibainisha kuwa kwa bahati mbaya kuna baadhi ya wateja hununua tiketi kwa mawakala ambao huwa hawapati taarifa kwa wakati kutokana na mawakala kuchelewa kutoa taarifa kwa abiria mapema.

“Sisi hatuna namba za mawasiliano ya wasafiri hao katika mfumo wetu wa mauzo. Tunawaomba wateja wetu wanaonunua tiketi kwa mawakala kuhakikisha wanaweka namba zao za simu katika mfumo wetu iii iwe rahisi kuwasiliana nao.

“Tunawaomba radhi wateja wetu kwa usumbufu uliojitokeza na tunaahidi kuendelea kuwahudumia kwa wakati.”




Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) nchini, Vickness Mayao (katikati), akikata utepe kuzindua mpango mkakati mpya wa miaka mitano wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuendelea kutekeleza program ya kukuza upatikanaji wa haki nchini kwa watu wote hususani wanawake na watoto. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng’wanakilala na Mwenyekiti wa Bodi ya LSF, Beng’i Issa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima pamba walalamikia mfumo

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAKULIMA wa pamba Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu wamemtaka mbunge wa jimbo hilo, Mhandisi Andrea Kundo kufanya marejeo na mapitio ya mifumo mizima inayotumiwa na Bodi ya Pamba katika ukataji wa fedha na ugawaji wa pembejeo za kilimo.

Pia wamemuomba mbunge kuwasaidia kufufua ama kuunda upya chama cha wakulima wa zao hilo, ili wapate chombo cha kuwasemea matatizo yao badala ya wao kulazimishwa kujiunga na Amcos, ambazo kwao wamedai haziwasaidii na badala yake zinawakandamiza na kuwanyonya.

Wakulima hao wamesema jana wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na mbunge wao katika Kata ya Mhango ambapo walisema kumekuwapo kwa changamoto kubwa ya kupata pembejeo nzuri na kwa muda mwafaka.

Charles Mwita alisema kuna changamoto kubwa ndani ya Bodi hususani katika mfuko wa pembejeo kwani mfuko huo umekuwa ukiwakata fedha za pembejeo, lakini wakulima wamekuwa wakikutana na tatizo la upungufu wa mbegu za kutosha na madawa mara mara .

Naye Maduhu Nila mkazi wa Mhango, alihoji kwa nini wakulima wamekuwa wakikatwa fedha ya pembejeo za mbegu na viuatilifu wakati mkulima akienda kuuza pamba yake badala ya kuwauzia pindi msimu unapoanza.

Baada ya kusikiliza kero hiyo, Mhandisi Kundo alisema changamoto hiyo imekuwa ya muda mrefu, na kwamba kuna uzembe wa baadhi ya viongozi wa juu ngazi ya wilaya wa kutofuatilia wala kutatua kero hiyo na baadhi yao wameonekana kunufaika na utaratibu huo.

“Haiwezekani ndani ya wilaya tukawa na watu wanaowachezea wakulima na kwa haraka nimegundua kuwa tatizo haliko kwa Amcos wala wasambazaji wa pembejeo hizo,” alisema Mhandisi Kundo.

Aliongeza kuwa analibeba na kwamba atawasiliana na wataalamu wa wizara hiyo, kufanya uchambuzi wa mifumo hiyo, ili iweze kupitiwa upya na kuboresha sekta ya kilimo.

“Nimekutana na malalamiko mengi sana juu ya usambazaji wa mbolea, mbegu na viuatilifu, nitaomba wizara kupitia upya mifumo hiyo, hasa kwenye zao la pamba ambalo wakulima wengi wamekuwa wakilalamika,” alisema.

Nae mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, David Masanja, alisema wakulima wamekuwa wakichezewa michezo mibaya, lakini ifikie wakati michezo hiyo iwe basi.

Alisema kwa kushirikiana na mbunge wake wanakwenda kusimamia na kutatua tatizo hilo, hivyo wakulima waondoe shaka kila kitu kitaenda sawasawa.

# LSF yaja na mambo 4 kuwapa haki wanawake

**Na Frank Monyo**

AFISA Mtendaji Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng’wanakila, ametaja maeneo makuu manne watakayotekeleza katika mpango wa miaka mitano katika shughuli zao za kusaidia upatikanaji wa haki pamoja na kuweka mazingira bora kwa wanawake kupata haki zao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mpango mkakati huo jana jijini Dar es Salaam, Ng’wanakila alainisha maeneo hayo kuwa ni Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za msaada wa kisheria, hususani kwa wanawake, kujenga uelewa kwa jamii juu ya Sheria na haki zao, hususani wanawake, kuboresha mazingira endelevu ya upatikanaji wa haki na kuimarisha taasisi na sekta ya msaada wa kisheria kuwa endelevu.

Alisema mpango huo umejikita katika kuchangia mpango wa Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG) SDG 16 uliolenga kuleta haki kwa wote na SDG 5 inayolenga kuboresha usawa wa kijinsia na kuwainua wanawake na wasichana.

Sambamba na malengo endelevu ya dunia, pia unachangia katika Mpango wa miaka 5 ya Maendeleo ya Taifa 2016/17-2020/2021, Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2025 utawala bora, Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Ukatili dhidi Wanawake na Watoto (NAP-VAWC), lengo kubwa ni kuondoa umaskini na kuchangia katika kuwezesha nchi kufikia katika uchumi wa kati.

“Leo tunayofuraha kuzindua mpango mkakati wa miaka mitano, ambao umelenga kutoa mwelekeo endelevu wa shughuli zetu nchini za kuwawezesha wananchi kupata haki zao”, alisema Ng’wanakila.

Aliongeza kuwa baada ya kukamilika kwa mradi wa ungwe ya pili 2016 -2020 ulioisha Desemba mwaka jana na kuendelea kwa mwaka mmoja hadi Desemba mwaka huu, mpango huo mpya wa miaka mitano utatoa dira na mwelekeo wa taasisi hiyo, huku kipaumbele kikiwa kusaidia upatikanaji wa haki na kuweka mazingira bora kwa wanawake kupata haki zao na kuchangia katika shughuli za uchumi na kuboresha maisha yao na familia zao.

Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Vickness Mayao, alisema amefurahishwa kuona kuwa LSF imekuja na mpango mkakati mpya wa miaka mitano na kusema inaonyesha kuwa programu ya upatikanaji wa haki itaendelea kutekelezwa, suala ambalo serikali inanufaika kwa kiasi kikubwa na matokeo yake.

**Leo tunayofuraha kuzindua mpango mkakati wa miaka mitano, ambao umelenga kutoa mwelekeo endelevu wa shughuli zetu nchini za kuwawezesha wananchi kupata haki zao.**



## Wenye ulemavu wahimizwa kupata chanjo ya corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Walemavu (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Hassan Sharifu, ametoa wito kwa watu wenye ulemavu kujitokeza kupata chanjo ya corona ili kujikinga na maambukizi.

Sharifu aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, kuhusu mwamko wa watu wenye ulemavu kuchanja chanjo hiyo.

Alisema wanapaswa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya na si kujijengea hofu dhidi ya chanjo hiyo.

"Mwitikio wa watu wenye ulemavu kuchanja chanjo umeonekana kuwa ni mdogo na watu wanashindwa kujitokeza kwa kujipa hofu zisizo na tija kwenye afya zao,"alisema.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema kuwa watu wenye ulemavu ni muhimu wakafuata maelekezo hayo kutoka kwa wataalamu wa afya na kuendelea kuchukua tahadhari kujilinda na ugonjwa huo.

Pia aliwataka watu wenye ulemavu kutojihusisha na mivutano iliyopo juu ya chanjo hiyo kwa kuwa usalama wa afya upo juu yao wenyewe.

"Ninawaomba wajilinde wenyewe, huku wakifuata maelekezo kutoka kwa wataalamu wa afya, hii ni pamoja na kujitokeza kuchanja chanjo hiyo ambayo serikali imekuwa ikitoa bure na hakuna sababu ya kuwa na hofu,"alisema.

Aliwaomba kuwajibika kwa kufanya kazi za uzalishaji pamoja na kuwapo kwa ugonjwa huo.

Alisema kuwa pamoja na kuwapo kwa ugonjwa wa corona wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii zitakazowaletea mapato badala ya kukaa majumbani kwa kisingizio cha kuhofia kuambukizwa.

Alisema hakuna sababu ya kukaa majumbani kwa hofu ya kuambukizwa ugonjwa huo.

# Waziri aijia juu TANESCO kisa kukata umeme ovyo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amepiga marufuku tabia ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kukata ovyo umeme kwa kisingizio kuwa gridi imehama.

Dk. Kalemani alitoa onyo hilo alipokuwa katika ziara yake ya kukagua kituo cha kufua na kupoza umeme cha Zuzu.

Alisema hivi sasa kuna tabia inayokera kwa watendaji wa Shirika hilo kukata umeme ovyo bila kutoa taarifa kwa wateja kwa kisingizio cha gridi kutoka.

"Hapa Dodoma umeme kukatia ni marufuku, lakini nashangaa juzi ulikatika ukiuliza unaambiwa eti gridi imetoka kwanini itoke na wewe upo hapo basi kuanzia leo tabia hii ikome kabisa kabla haijaondoka na mtu," alisema Dk. Kalemani.

Alisema hivi sasa Mkoa wa Dodoma upo umeme wa kutosha kutokana na kuwapo kwa kituo cha kufua umeme cha Zuzu ambacho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati za umeme zaidi ya 600.

Alisema mahitaji ya umeme kwa Dodoma hivi sasa ni Megawati 48, na yamekuwa yakipanda kila siku hivyo kituo hicho kitakuwa mkombozi kwa kuwa na umeme wa uhakika.

"Kituo hicho kinafua na kupoza umeme na kusambaza katika Mkoa wa Singida lakini baadaye kitatumia pia kupeleka nchini Zambaia na Kenya,"alisema Dk. Kalemani.

Akizungumzia matukio ya kuungua kwa vituo vya kufua na kupozea umeme nchini, Waziri huyo alisema ipo haja ya kuwekwa sawa mifumo ya kubaini tatizo linaweza kujitokeza ili hatua zichukuliwe kabla ya kutokea.

"Lile tatizo la kituo cha kupoza umeme lililotokea hivi karibuni mkoani Morogoro tayari nimeshaunda tume ili kubaini kama ilikuwa bahati mbaya au makusudi," alisema. Aidha, alisema ili kukomesha hali ya kuungua kwa vituo hivyo TANESCO inatakiwa kuajiri watumishi wenye uzalendo na wenye weledi katika nafasi hiyo.

"Hivi vituo ndipo umeme wote unatoka hapa tuweke watu wazalendo, wenye weledi na asiwe mlevi na nikikuta mtu mlevi yeye na aliyemwajili wote wataondoka na pia tusitumie raia wa kigeni hawa wanaweza kutuingiza chaka," alisema Dk. Kalemani.

Naye, Meneja wa Mradi wa kituo hicho cha kufua umeme cha Zuzu, Newton Mwakifwamba, alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika Septemba 27, mwaka huu.

"Mradi upo asilimi 98, za kukamilika na tunatarajia hadi kufikia Septemba 27, mwaka huu kuwa umekamilika na unaghalimu Dola za kimarekani milioni 53," alisema Mwakifwamba.




Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remedius Mwema, akizungumza na wananchi wa Mji mdogo wa Kibaigwa, wilayani humo, mkoani Dodoma juzi, alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bunge lajitosa sakata la Bodi ya Walimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BUNGE limeahidi kushauriana na serikali kuhusu uwapo wa Bodi ya Kitaaluma ya Walimu na Tume ya Utumishi ya Walimu kwa kuwa suala hilo linapingwa na wadau kwa madai kuwa linamkomoa mwalimu kimaslahi na si kumsaidia.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akifungua kongamano la walimu wenye ulemavu nchini lililoandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

Alisema watashauriana na serikali ili kuwapunguzia walimu mzigo wa makato ya asilimia za fedha kila mwezi.

"Awali wakati chombo hicho kinapitishwa tulidhani kingewasaidia katika shughuli zao za kiutendaji, lakini kumbe kimeonekana kuwakandamiza hususani katika maslahi yao," alisema.

Alisema walimu ni watu muhimu sana katika jamii kwa kuwa kila kiongozi amepitia mikononi mwao na Bunge lipo tayari kuhakikisha wanalisimamia suala hilo.

Kuhusu suala la miundombinu ya walemavu, alisema serikali itaendelea kulifanyia kazi na bungeni wamekuwa wakisisitiza kila siku miundombinu inayojengwa ya shule izingatie watu wenye ulemavu.

Kwa upande wake, Katibu wa CWT, Deus Seif, aliomba Spika kufikisha ombi serikalini suala la wasiopungua 59,000 ambao wakati wa uhakiki wa vyeti feki walikuwa wamepandishwa vyeo lakini kupitia zoezi hilo walinyang'wanywa barua na hawajapandishwa vyeo.

Aliomba wanafunzi wenye ulemavu wapewe ruzuku sio mikopo.

Naye, Rais wa CWT, Leah Ulaya, alimpongeza Spika wa Bunge kutokana na kuonyesha weledi katika kazi za kulisimamia Bunge hilo.

Alisema wanaamini yale waliyoyaomba yatakwenda kufanyiwa kazi kwa sababu Bunge ni moja ya muhimili wa taifa.

Akizungumza kwa niaba ya walimu wenye ulemavu, Ulumbi Shami, alimuomba Spika kuhakikisha anayasimamia maombi yao hususani ya urekebishwaji wa miundombinu ya watu wenye ulemavu ili iwe rafiki.





# TAWCA yamkosha Rais Mwinyi kuandaa viongozi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekipongeza Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania (TAWCA) kwa jitihada zao katika kuandaa viongozi bora wanawake wanaotoa mchango kwa maendeleo ya Taifa.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alieleza hayo kupitia hotuba aliyoisoma kwa niaba ya Rais Dk. Mwinyi katika ufunguzi wa kongamano la nne la TAWCA lililofanyika jijini Zanzibar.

Hemed alisema amefurahishwa na mikakati iliowekwa na chama hicho katika kuhakikisha wanalisaidia taifa, kwa kuandaa viongozi mbalimbali wanawake ambao wamekuwa wakitoa mchango wao katika kukuza uchumi wa nchi.

Alieleza kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kuthamini mchango wa chama hicho kutokana na kufanya kazi nzuri katika kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika kujitolea na kuleta maendeleo.

Makamu wa Pili wa Rais alisema Tanzania ina viongozi wengi wa kupigiwa mfano ambao wameweza kushika nafasi mbalimbali kitaifa na kimataifa, kutokana na uwezo walionao, jambo ambalo limetoa imani kubwa kwa jamii, kwa viongozi wanawake.

Kutokana na mchango mkubwa waliouonyesha kwa Taifa, aliwahakikishia kuwa serikali itaendelea kuwaamini wanawake kwa kuwapa fursa mbalimbali za uongozi.

Kupitia hotuba hiyo Hemed aliwaasa wahasibu hao kuendelea kuwashawishi na kuwahamasisha wanawake wengi zaidi kujiunga na elimu ya juu kwa kusomea fani hiyo, ili miaka ya mbele nchi iwe na wataalamu wengi wanawake ambao taifa linategemea kwa kiasi kikubwa mchango wao.

Naye, Mwenyekiti wa chama hicho, Dk Neema Kiure Msussa, alieleza kuwa TAWCA katika kuwawezesha wajasirimali wanawake, imesaidia jumla ya wanawake 101 kwa kuwapatia elimu pamoja na kuwapa mafunzo na mitaji, kwa ajili ya kuimarisha harakati zao za kimaisha kupitia biashara.

Alisema kwamba chama hicho kimetanua wigo kitaifa na kimataifa kwa kujiunga na vyama mbalimbali vya wahasibu wakiwa na lengo la kupata uzoefu kutoka kwa wataalamu tofauti kutoka mataifa mengine.

Akiwasilisha salamu kutoka Hospitali ya Aga Khan katika kongamano hilo, Dk. Erine Kitege alieleza kuwa katika kongamano hilo wataalamu kutoka hospitali hiyo watafanya vipimo vya saratani ya shingo ya kizazi na saratani ya matiti kutokana na kinamama kuathiriwa sana na ugonjwa huo.

Dk. Kitege alieleza kuwa asiliamia 75 ya kinamama hawafiki hospitali kwa wakati kupata huduma ya tiba ya saratani, hivyo kuathirika kiafya.



Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Commodore Azana Msingiri, akishika samaki waliovuliwa na wavuvi wa KMKM, kwa kushirikiana na washirika wao Kampuni ya Wisam, Mtoni mjini Zanzibar jana, ikiwa ni majaribio ya uvuvi wa bahari kuu kwa lengo la kuunga mkono sera ya uchumi wa bluu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# KMKM yajitosa rasmi uchumi wa bluu

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

KIKOSI Maalum Cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeanza majaribio ya meli yake kuvua katika uvuvi wa bahari kuu, ili kuendana na azma ya Serikali ya Zanzibar ya uchumi wa bluu.

Meli hiyo imefanikiwa kuvua tani zaidi ya tano za samaki ikiwa ni mara ya kwanza kuanza kuvua katika bahari kuu.

Akiwa katika mapokezi ya meli hiyo, Mkuu wa KMKM, Commodore Azana Msingiri, alisema kurudi kwa meli hiyo kunaashiria kuanza kwa neema katika kikosi hicho kupitia uchumi wa bluu.

Alisema meli hiyo imerudi na samaki wakubwa na wenye kiwango, ambao watapatikana katika kikosi hicho na lengo la kikosi hicho ni kuuza kwenye soko la kimataifa

Msingiri aliwataka wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kujitokeza kikosini kwake kufanya biashara hiyo.

Naye Mkuu wa doria wa KMKM, Kamanda Hussein Ali Mwinyi, alisema kwa majaribio yaliyofanyika ya meli hiyo ni ishara nzuri kutokana na samaki waliopatikana pamoja na chombo hicho kuanza kazi ingawa hali ya hewa haikuwa shwari.

"Hali ya hewa kwa sasa baharini sio nzuri sana, lakini tushukuru tumefanikiwa kupata samaki wengi ikiwa ni mwanzo mzuri," alisema.

# Watakiwa kushiriki sensa ya mwakani

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makaazi Zanzibar, Balozi, Mohammed Haji Hamza, amewataka wananchi kushiriki kikamilifu Sensa ya Watu na Makazi linalotarajiwa kufanyika mwaka 2022, ili kuiwezesha serikali kufikia lengo ililojiwekea.

Hayo aliyaeleza alipofanya ziara ya mikoa mitatu ya Unguja yenye lengo la kuhamasisha na kuangalia maeneo yaliopangwa kufanyika sensa ya majaribio mwezi ujao.

Alisema, matokeo ya sensa hiyo ya awali yataiwezesha serikali kupata takwimu za msingi zinazotumika kuakisi hali halisi iliyopo kuelekea sensa kuu, kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo, kutunga sera kufuatilia utekelezaji wake.

Alisema ni muhimu wananchi watoe ushirikiano kwa wakusanya takwimu, ili kuliwezesha zoezi hilo kwenda vizuri na kuleta matokeo tarajiwa kwa maendeleo ya nchi.

Hivyo, aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya na masheha kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa sensa kwa wananchi, ili kuwaweka tayari kushiriki zoezi hilo kwa maendeleo ya taifa na watu wake.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sensa ya Watu na Makazi ni miongoni mwa sehemu muhimu katika maendeleo ya wanajamii na mustakabali wa nchi kimaendeleo.

Alisema, sensa ya mwaka 2022 itakuwa ya kipekee, kutokana na aina ya madodoso na teknolijia ya kisasa ya kukusanya taarifa kwenye ngazi mbalimbali na kuainisha changamoto na kupanga namna bora ya kuzitatua.

"Sensa ya watu na makazi lengo lake ni kupata idadi kamili ya watu kwa lengo la kupanga maendeleo na kukuza uchumi," alisema.

Alisema, sensa hiyo itakuwa ya kipekee kwa kuwa itatumia teknolojia ya hali ya juu, ili kupata taarifa kuanzia kwenye ngazi ya kaya, shehiya, wilaya na mikoa kwa kukusanya taarifa sahihi za idadi ya watu, umri, elimu na upatikanaji wa huduma za kijamii kama maji, umeme na afya.

"Kukamilika kwa sensa ya watu na makazi kutaimarisha na kupanga mipango ya maendeleo ya kitaifa, kupima matokeo na kufuatilia uwajibikaji katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya taifa."

Alisema, kutokana na zoezi la sensa kuwa tegemeo la taifa, kila mwananchi anawajibika kutekeleza jukumu lake la msingi kwa kushiriki zoezi hilo.

"Kila mmoja kwa mujibu wa nafasi aliyonayo, ahakikishe anatumia nafasi yake kuihamasisha jamii kushiriki zoezi hilo.

Alisema huduma za maendelo ya kijamii na kiuchumi katika nchi zinahitaji kujulikana kwa idadi sahihi ya wananchi na kujua mahitaji ya nguvu kazi pamoja na kutumia malighafi zilizopo.

Aidha, Balozi Hamza, alisema, sensa hiyo itaiwezesha pia serikali kujua huduma zake itazitoa vipi, hivyo, zoezi hilo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo.

Sensa ya majaribio itajumuisha jumla ya maeneo 10 katika mikoa yote ya Zanzibar.

Baadhi ya maeneo hayo ni Shehiya ya Bumbwini Misufini Kijiji cha Kidutani, Sharifumsa, Magharibi 'A', Ndijani Mseweni Wilaya ya Kati, Shehiya ya Nganani, Kijiji cha Kiovya Wilaya ya Kusini na Kilindi, Mkoa wa Kaskazini Unguja.



**LIL WAYNE ATOBOA SIRI ZA UTOTONI** Uk.14

JUMAMOSI AGOSTI 21, 2021

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



## NANCY SUMARI
# Kutoka Miss Tanzania 2005 hadi uandishi

UNAMKUMBUKA mlimbwende Nancy Sumari? Jina lake linazidi kuvuka katika masikio ya Watanzania, sio tu kwa tasnia ya urembo, bali kwa kipaji chake cha uandishi wa vitabu.

Nancy ambaye alikuwa mshindi wa shindano la Miss Tanzania mwaka 2005, alifanya vizuri katika Miss World baada ya kushika namba mbili na kumjengea sifa kemkem ndani na nje ya nchi.

Sumari amefanya mahojiano maalum na BT hivi karibuni, amesema safari yake kuanzia katika ulimbwende hadi uandishi wa vitabu imekuwa ya kushangaza, lakini ndani yake kuna mafanikio.

Anasema katika maisha ya uandishi, amefanikiwa kuandika vitabu vitatu kikiwamo cha alichokiita jina la Samia, ambacho kinaelezea historia ya Rais Samia Suluhu Hassan, alichokizindua juzi.

**CHIMBUKO LA KUPENDA VITABU**

Anasema mapenzi yake ya kupenda kusoma vitabu yalianzia nchini Kenya katika shule ya Shepherds Junior akiwa darasa la sita hadi la saba kati ya mwaka 1998-1999 .

Akiwa shuleni hapo kuna wakati alikosa ada kwa wakati, hivyo alitakiwa kushinda maktaba kujisomea wakati wenzake wakiwa darasani.

Anaeleza kuwa shule hiyo ukikosa ada haurudishwi nyumbani unatakiwa kwenda kujisomea maktaba, hivyo kitendo hicho kilimjengea kupenda kusoma vitabu na kupenda kufuatilia mwendelezo wa hadithi.

"Sikuwahi kujiona kama nitakuwa mwandishi nilikuwa napenda vitabu nilipokuwa shule,kuna wakati wazazi wangu waliyumba kiuchumi yaani ada ilikuwa inasuasua kwa hiyo shuleni walichokuwa wanafanya kuliko kukufukuza urudi nyumbani wanakuambia uende maktaba,"anasema Sumari.

**SABABU YA KUANDIKA KITABU**

Sumari anasimulia kwamba sababu zilizomfanya kuandika kitabu cha Samia, ni kuvutiwa na kiongozi huyo ambaye ameweka historia nchini kwa ujasiri wake.

Anasema ndani ya kitabu hicho ameelezea changamoto mbalimbali alizozipitia, hivyo ameona kumuenzi na kumsherehekea kwa kujifunza kupitia hadithi ya maisha yake.

"Ninaamini binti yoyote wa Kitanzania, kiaafrika na Dunia akisoma kitabu hiki anaweza kuhamasika na kuwa na mtazamo tofauti katika kuamini katika kazi, uzoefu na kukubali kushirikiana na watu mbalimbali ili kufikia malengo fulani,".anasema Sumari.

Anasema alianza kuandika kitabu hicho wakati wa kifo cha aliyekuwa Rais John Magufuli, baada ya kuona Rais wa awamu ya sita Samia Suluhu Hassan, akiapishwa lilikuwa ni tukio la kihistoria nchini.

"Ile siku ilikuwa ya kihistoria nikaanza kulitazama kwa jicho pana kwamba kwa mtoto aliyezaliwa hizi zama hataweza kuelewa ukubwa wa tukio anaweza kuliona ni tukio la kawaida, lakini ni la kukumbukwa,"anaeleza.

BASI SAWA

## Msami akubali cha zamani kinalika



JE, una moyo mgumu kiasi ambacho unaweza kumsaidia mpenzi wako wa zamani? Basi kwa Irene Uwoya, jambo hilo kwake ni rahisi sana.

Kulingana na Msami Baby, amesema jambo la kusaidiana halijali uhusiano, kwani yeye alisaidiwa na Uwoya wakati alipokamatwa na polisi kutokana na kusababisha ajali ya barabarani.

"Mimi na yeye ni washkaji tu, nakumbuka kuna siku nilipata ajali ya gari usiku, asubuhi nikawa polisi hivyo nikawa sipo vizuri mfukoni kwa haraka haraka nikampigia simu Irene Uwoya akanitumia laki tano," amesema.

## Kiba sasa hizo sifa



SASA imekuwa sifa! Kwani msanii nyota wa muziki wa Bongo Fleva, anatarajia kuachia ngoma mpya ambayo ndani yake kuna mwanamuziki mkali Maud Elka.

Wimbo huo ambao unasubiliwa na mashabiki wake utakuwa remix ya wimbo wa 'Songi Songi' aliouimba Maud Elka akishirikiana na Hiro.

Baadhi ya mashabiki wake wamefurahishwa na ujumbe wa msanii huyo kupitia katika akaunti yake ya Twitter, akiwataka kupokea wimbo huo, ambao wengi wameonekana kupagawa huku wakitaka kusikia ladha ya kibao hicho.



## Mwe! Gigy Money mapenzi ya gwala

MWANAMUZIKI wa bongo Fleva, Gigy Money, amesema huwa hana aibu kumfuata mwanamume anayempenda.

Amesema endapo akikataa atafanya kila mbinu ukiwamo kumkamata mashati hadi akubali, kwani anachukia suala la kushindwa hasa katika mapenzi.

"Mimi kama nikimpenda mwanamume sina aibu kumfuata na kumwambia ninavyojisikia, akitakataa nitamshika shati lazima utaenda tu, mimi ndio Gigy Money," amesema.



## Amber Rutty eti hizo ni kiki?

BAADHI ya mashabiki wa mpambaji wa video za muziki, Amber Rutty, wamesema alichozungumza msanii huyo kwamba alipigwa na mume wake hadi kuharibu nyumba ni sehemu ya kiki walizozioea.

Amber Rutty, amedai alipigwa na mumewe Davil na kumsababishia kumpoteza mtoto tumboni kutokana na wivu aliokuwa nao dhidi ya mwimbaji Enock Bella.

Katika mahojiano yake na EATV, Amber Rutty amesema sababu zilizofanya kupigwa na mumewe ni kufumwa na ujumbe mfupi katika simu yake alizokuwa anawasiliana na msanii Enock Bella ambaye anadai alikuwa anamtongoza.

## Ajali zilivyopoteza mastaa Bongo

Na Adam Fungamwango

TANZANIA ni moja kati ya nchi zilizojaaliwa kupata wasanii na wanamuziki wakubwa mahiri na tishio kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Si kwenye muziki wa dansi, taarabu, bongo fleva, na hata waigizaji, Tanzania imebahatika kupata wanamuziki ambao wameipatia heshima kubwa nchi hii kwenye masuala la muziki.

Hata hivyo kwa bahati mbaya wengi wao wamefariki kwa sababu mbalimbali, ikiwamo maradhi na ajali.

Leo tutawaangalia wanamuziki na wasanii bora kabisa nchini, ambao walifariki dunia kutokana na ajali za barabarani.

**SALUM ABDALLAH**

Ni mmoja wa waasisi wa muziki wa Tanzania. Salum Abdallah alizaliwa mwaka 19 mwaka 1928 mjini Morogoro kwa baba Mwarabu raia wa Yemen na mama mwenyeji wa mkoa wa Morogoro.

Licha ya kwamba alifariki mwaka 1965, lakini baadhi ya nyimbo zake ni maarufu hadi leo. Nyimbo hizi ni 'Mkono wa Idd', 'Shemeji Shemeji huku Mwazima Taa, ' Wanawake Tanzania', 'Ngoma Iko Huku', 'Nina Mpenzi wangu Kibambaye' na nyingine nyingi.

Alifariki mwaka 1965 kwa ajali ya gari, baada ya lori lake la mchana alilokuwa akiendesha kugonga ukingo wa daraja na kumtupa nje. Ajali hiyo ilitokea mkoani Morogoro wakati alipotoka kulikwamua lori hilo lililokuwa limekwama na kulirudisha nyumbani.

**MBARAKA MWINSHEHE**

Huyu pia ni mwanamuziki aliyetokea Morogoro kama Salum Abdallah. Ni mwanafunzi wa Salum pia. Alizaliwa Moro mwaka 1944 na kutokea kuwa mwanamuziki mkubwa mno Afrika Mashariki na Kati.

Alikuwa mwimbaji na mpiga gitaa kwenye bendi ya Moro Jazz, na ilipofika mwaka 1973, aliunda kundi lake la Super Volcano. Moja ya wimbo wake bora ambao hadi leo unapendwa na vijana kwa vya sasa no 'Shida'.

Alifariki Januari 12, 1979 Mombasa nchini Kenya alipokuwa amekwenda kwenye kazi zake za muziki.

Gari dogo la rafiki yake alilokuwa amepanda liligonga lori lililokuwa limeegeshwa na kufariki dunia.

**ABUU SEMHANDO 'BABA DIANA'**

Ni mwanamuziki mkongwe, mpiga drums wa bendi za Tanga International, Super Matimila, Tomatoma, Vijana Jazz na mwishowe African Stars 'Twanga Pepeta'.

Alifariki dunia usiku wa kuamkia Desemba 18, 2010, baada ya pikipiki alilokuwa akiendesha kutoka kwenye onyesho la Twanga Pepeta, kugongwa na gari eneo la Mbezi Beach, Dar es Salaam na kusababisha kifo chake.

**ISSA KIJOTI**

Mwimbaji wa muziki wa taarabu aliyekuwa akichipukia, baada kutoa wimbo wake wa 'Usinijadili' ambao ulikuwa na kionjo kilichoondokea kuwa maarufu kilichoimbwa hata na watoto mitaani 'nichumu, nichumu tena, mwaaa', Issa Kijoti, alifariki dunia 2011, baada ya basi dogo walilokuwa wakisafiria kutoka Mbeya walikokwenda kimuziki, kugonga lori lililokuwa na mbao, ambalo basi hilo lilitaka kulipita mkoani Morogoro.

Kijoti, aliyekuwa kiongozi wa Five Star na maarufu wakati huo, alifariki dunia na baadhi ya wanamuziki wenzake.

**SHARO MILIONEA**

Ndiyo alikuwa ameshaanza kuwa maarufu na kuanza kupata mafanikio ya kazi yake ya uigizaji wa ucheshi.

Sharo Milionea, jina halisi Hussein Ramadhani, wakati aanza kuonja mafanikio, baada ya msoto wa kufika hapo, alipata ajali mwaka 2012 katikati ya maeneo ya Segera na Muheza. Akiwa anakwenda kwao mkoani Tanga, gari alilokuwa akiendesha aina ya 'Toyota Harrier' alipokuwa akitoka kwenda Muheza, lilipinduka baada ya kuacha njia kwenye eneo linaloitwa 'Maguzonizonga', na kusababisha kifo chake.





## Hukumu ya Tuli; Hamu ya mfalme, maafa na ukame

Na Adam Fungamwango

FILAMU inaitwa 'Hukumu ya Tuli', lakini mashabiki wake ambao waliiangalia na kuipenda wakaipa jina la 'Hamu ya Mfalme'. Ni filamu ambayo inaonyesha jinsi baadhi ya viongozi wanaotumia madaraka yao vibaya, wakileta mambo ya ubinafsi na upendeleo kiasi cha kusababisha matatizo kwa wananchi wanaowasimamia.

Imechezwa na wasanii Lisah Hellah, Tausi Hellah, Ester Hellah, Halima Mkukutika, Juma Iligo, Tabu Hassan, Mzee Kofi, Sadiki Shilla, Amir Mtambo, Charles Steven na wengineo.

Inaanza kuonyesha mfalme kwenye himaya moja, akitembea na walinzi wake. Njiani alikutana na msichana mmoja mrembo. Anawauliza walinzi wake alikotokea. Wanamjibu kuwa ni binti wa mzee Mponda. Mfalme anaonekana kuvutiwa na binti huyo, hivyo anawaamuru wakamwite baba yake mzazi. Mzee Mponda anafurahi, naye anampelekea habari mkewe. Mkewe naye anaona bahati illoje, anampasha binti yake Tuli. Badala ya kufurahi kuwa malkia, anakataa kuwa mke wa mfalme kwa madai ana mpenzi wake ambaye ni Nungini.

Kama ilivyotegemewa, kukataliwa kulimkasirisha mfalme ambaye aliamua kuchukua hatua za haraka kwanza kumtisha Nungini na familia yake.

Dada anamuweka chini kaka yake na kumwambia aachane na mpango wa kumuoa Tuli kwani mfalme ameshaingia kati na hawezi kumfanya lolote, zaidi ya kuambulia kifo tu.

Mpango unaokubaliana hapo ni yeye kukimbia aende mbali na himaya hiyo ili kuepuka hifo. Nungini anatoka na kwenda kumuaga mpenzi wake Tuli. Tuli anamkataza asiondoke, lakini Nungini anamwambia yeye anaondoka kwa sababu hawezi kuona kwa macho yake, akiolewa na mtu mwingine. Ataumia sana. Anatoroka. Walinzi wanatumwa kwenda kumuua Nungini. Hawamkuti. Wanamkuta dada yake na kumuua. Tuli anaolewa kwa lazima na mfalme. Siku ya harusi, Tuli anaanguka na kufariki dunia.

Kifo chake kinaleta simanzi kubwa kwenye himaya nzima kuanzia kwa mfalme, hadi kwa watawaliwa. Nungini anarejea kwa sababu hakukuna na hatari tena. Mzimu wa Tuli unaanza kuwatokea wananchi wa himaya hiyo, sehemu mbalimbali. Mwishoni unalipiza kisasi kwa kumuua mfalme na walinzi wake.

Wanaamua kufanya tambiko. Tuli anatokea na kuahidi hatowadhuru na kuwatokea tena, lakini aliahidi kuwa ataishi na Nungini popote pale, kwa shida na raha na ndiye mwanamume anayempenda pekee, hivyo ataondoka naye. Akamshika mkono. Wakatoweka.

# Lil Wayne atoboa siri za utotoni




NYOTA wa muziki Rap wa Marekani, Dwayne Carter Jr, maarufu kama Lil Wayne, ameistua dunia baada ya kuweka wazi kwamba akiwa na umri wa miaka 12 alijaribu kujiua kutokana na kutawaliwa na upweke.

Staa huyo wa muziki amesema hayo wakati akizungumzia kuhusu matatizo ya afya ya akili na mtangazaji Emmanuel Acho, kwenye kipindi chake cha mazungumzo.

"Wakati hauna mtu wa kumwendea, hakuna mtu wa kupata habari, huwezi kuwa na marafiki wako shuleni kwa sababu bado unajaribu kuwa mzuri kwao ni jambo gumu na zito. Nikiwa na umri wa miaka 12 nilijaribu kujiua kuondokana na tatizo hili," amesema.

Wayne amesema alijitahidi kwa miaka miwili ya ujana wake hadi mama yake alipogundua alikuwa akitoroka shule.



## Mke wa Paul Okoye aomba talaka

MKE wa msanii maarufu wa Nigeria, Paul Okoye, amewasilisha mahakamani ombi la kudai talaka.

Anita Okoye, amewasilisha hati hiyo mahakamani akiomba ndoa yao ivunjwe baada ya wawili hao kutengana.

Kulingana na mtandao wa Pulse, Anita amelalamika suala hilo alimshauri pia mumewe, lakini alionekana kukasirika.

Uvumi wa wawili hao kutaka kupeana talaka ulianza Aprili, mwaka huu wakati iliripotiwa kwamba alihama na watoto wao watatu kwenda Marekani.

## Dababy kumbuka hasira hasara

UKISIKIA Mambo yanaenda kombo ndio huku! Kwani rapa mkali kutoka marekani, Dababy, ameamua kuachana na muziki huo baada ya wanaoandaa matamasha ya muziki kumsusa.

Dababy amepigwa marufuku kushiriki matamasha sita makubwa baada ya kauli yake aliyoitoa kwenye tamasha la ROLLING LOUD, lililofanyika July 25 mwaka huu kutafsiriwa ni ya kibaguzi.

Dababy amedai ameamua kuachana na Rap baada ya kupost kwenye instastory yake akiimba kionjo cha wimbo RnB na kusema maneno yaliyoibua hasira kwa waandaaji.





## Silento nenda mahakamani kama kidume

RAPA wa Marekani Ricky Hawk, maarufu kama Silento, amefunguliwa mashtaka ya mauaji ya ndugu yake.

Kwa mujibu wa taarifa, mwili wa ndugu yake huyo, Rooks, ulikutwa mwanzoni mwa mwaka huu ukiwa na majeraha ya risasi.

Mwanamuziki huyo alifunguliwa mashtaka matano Agosti 3, mwaka huu, ukiwamo kupanga na kutekeleza mauaji, utesaji na kukwepa kusema ukweli.

## Doris Chima afariki dunia

MSANII mkongwe wa Nollywood, Doris Chima, amefariki dunia baada ya kuugua ugonjwa wa saratani kwa muda mrefu.

Mwekiti wa wasanii wa Nigeria, katika jimbo la Logos, Emeka Rising Ibe, amethibitisha kutokea kwa kifo hicho na kusema alizungumza naye kuhusu afya yake wiki iliyopita na kumwambia anajisikia vyema.

"Aliniambia wiki iliyopita kuhusu afya yake na kuniambia anaweza kuondolewa katika tiba yake ya mazoezi, nimevunjika moyo kama mwanachama wetu kuondoka nasi," amesema.



**MAKALA**

# Bilioni 985 zifanikishe mageuzi elimu ya juu

Na Reubeni Lumbagala

TAIFA halina budi kuwekeza vya kutosha katika elimu ya juu ili kuongeza kasi ya maendeleo ya wananchi na kukuza uchumi. Uwekezaji wa elimu ya juu ni lazima uzingatie ujenzi wa miundombinu ya kutolea elimu yaani kuboresha kumbi za mihadhara, majengo ya utawala, ujenzi wa maabara, karakana, maktaba, mabweni ya wanafunzi, vyumba vya kompyuta na kuziweka za kutosha bila kusahau huduma za kijamii kama maji safi na salama.

Vilevile, mageuzi katika elimu ya juu yanakwenda sambamba na kusomesha wahadhiri wa kutosha ndani na nje ya nchi, bila kusahau kuongeza fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ili kuongeza wigo wa wanufaika, hatimaye kupata rasilimaliwatu wa kutosha kusaidia jitihada za kujiletea maendeleo katika Taifa.

Katika jitihada za kuboresha sekta ya elimu nchini hasa elimu ya juu, serikali imeasisi Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi unaogharimu dola milioni 425 (takriban Shilingi bilioni 985) kutoka Benki ya Dunia (WB).

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe, akiwa katika ziara ya kikazi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) mkoani Iringa ana sema ndani ya miaka mitano wamepata mradi mkubwa chini ya Benki ya Dunia ambao ni wa elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi.



Miundombinu ya kisasa kwa ajili ya kutoa huduma bora na muhimu za elimu kama majengo ni moja ya mategemeo ya wananchi katika mradi huo wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi. **PICHA ZOTE :MTANDAO.**

"Mradi huu utatekelezwa katika vyuo vyote vya umma pamoja na vishiriki, Tume ya Vyuo Vikuu, Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa vyuo vikuu, mafunzo kwa wafanyakazi waliokazini" anasema Profesa Mdoe.

Aidha, mradi huo utawezesha ujenzi wa miundombinu bora na ya kisasa, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kusomesha wahadhiri ndani na nje ya nchi na pia kupeleka watumishi kwenye mafunzo ili waendanea na mahitaji ya sasa.



Uboreshaji na mageuzi katika elimu ya juu hauna budi kufanyika kutokana na ukweli kuwa ufaulu wa wanafunzi wanaohitimu kidato cha sita umekuwa ukiongezeka mara dufu, hali inayopelekea mahitaji makubwa ya nafasi za kujiunga na elimu ya juu kila mwaka. Mathalani, katika matokeo ya kidato cha sita mwaka 2021, ufaulu umeimarika kwa asilimia 0.19 kutoka asilimia 97.74 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 97.93 mwaka huu (2021).

Ongezeko kubwa la ufaulu wa wahitimu wa kidato cha sita na wale wa ngazi ya stashahada katika fani mbalimbali wanaotaka kujiendeleza katika elimu ya juu yaani shahada ya kwanza, kunaongeza mahitaji ya miundombinu na rasilimali watu wa kuwahudumia wawapo vyuoni. Ndiyo maana maboresho na mageuzi ya kimiundombinu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kusomesha wahadhiri, ni jambo lisiloepukika katika mazingira ya sasa ya utoaji wa elimu ya juu katika vyuo mbalimbali nchini.

Kimsingi, Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi utapunguza kwa kiasi kikubwa mahitaji katika taasisi nyingi za umma za elimu ya juu.

Aidha, katika fedha hizo, bilioni 100 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kilichopo Butiama mkaoni Mara.

Sanjari na hilo, progamu mpya 290 zitaanzishwa, huku wahadhiri 623 wakitarajiwa kusomeshwa. "Tutasomesha wahadhiri zaidi ya 623 wa Shahada ya Uzamivu na 477 wa Shahada ya Umahiri, tutaanzisha Programu mpya 290 tutaongeza udahili wa wanafunzi lengo kuwabeba hawa wanafunzi ambao wanaongezeka" anasisitiza Prof. Mdoe.

Vilevile, katika kuchagiza maendeleo ya elimu ya juu na hatimaye maendeleo ya kiuchumi, wizara ya elimu katika bajeti ya mwaka 2021/2022, imeongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu na kufikia bilioni 570 kutoka bilioni 464, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 106.

Anasema bilioni 570 zinalenga kuwanufaisha wanafunzi 160,000 ambapo kati ya hao, wanafunzi 62,000 ni wa mwaka wa kwanza na 98,000 ni wale wanaoendelea na masomo. Huu ni uwekezaji mkubwa ambao utawasaidia wanafunzi wengi hasa wanaotoka familia maskini ambao wanategemea sana mikopo ili kumudu gharama za masomo na maisha kwa ujumla wawapo vyuoni.

Kwa ujumla, mradi huu utaleta manufaa makubwa kwa taifa kutokana na kuzalisha wahitimu bora wenye maarifa, ujuzi na stadi muhimu zinazohitajika kwa maendeleo ya nchi hasa katika nyanja ya sayansi, teknolojia, uhandisi, afya, kilimo, mifugo, uvuvi, fedha, na maendeleo ya viwanda kwa ujumla ambapo fani hizi ni muhimu sana katika kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati juu.

Ni vyema waliopewa dhamana kusimamia fedha hizi katika shughuli kama vile ujenzi na manunuzi ya vifaa kuwa wazalendo hasa ili fedha hizo ziweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa kwa kuzingatia thamani ya fedha, hatimaye taifa lipige hatua zaidi katika elimu na uchumi pia.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali ya wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: 0620-800462.**

# MULLAH ABDUL BARADAR

## ●Mtaliban aliyeongoza mapigano hadi ushindi
## ●Alikamatwa na Marekani, aliachiwa kuleta amani



Kiongozi wa Taliban, Mullah Abdul Baradar, akifanya mazungumzo na ofisa wa kundi la Hamas la palestina, Mousa Abu Marzook, nchini Qatar. **PICHA : MTANDAO.**

**Na Mwandishi wetu**

DUNIA imetaharuki, mataifa makubwa yameachwa mdomo wazi wakiangalia kile kinachotokea nchini Afghanistan baada ya kundi la Taliban, kuchukua madaraka.

Ilikuwa kama similizi za kutisha baada ya wanamgambo kuripotiwa kuchukua maeneo mbalimbali ya nchi hiyo, baada ya wanajeshi wa Marekani na washirika wake kuondolewa na kuiacha serikali ya nchi hiyo, ikiwa haina la kufanya kutokana na kukosa vikosi imara vya kujilinda.

Bila kupata upinzani mkubwa, wanamgambo wa Taliban waliteka miji ya mikoa na hatimaye waliingia mji mkuu wa Kabul, na kuiondoa serikali madarakani bila kipingamizi chochote.

Hata hivyo, katika ushindi huo ambao unaangaliwa kwa macho makini na mataifa mbalimbali, yupo kiongozi wao mahiri, Mullah Abdul Ghani Baradar, ambaye anatajwa kuwa ni mmoja ya watu wanne walioanzisha kundi hilo mwaka 1994.

Baradar, alipanda ngazi na kuwa mtu muhimu wa kundi hilo baada ya Taliban kuangushwa katika vita iliyoongozwa na Marekani mwaka 2001.

Hata hivyo, alikamatwa na vikosi vya arekani wakishirikiana na Pakistan akiwa eneo la kusini mwa mji wa Pakistan wa Karachi mwezi Februari mwaka 2010.

Kuanzia hapo, Baradar hakusikika tena hadi mwaka 2012 wakati jina lake lilipoorodheshwa katika orodha ya wafungwa wa Taliban ambao serikali ya Afghanistan ilitaka kuwaachilia kama njia ya kuvutia mazungumzo ya amani.

Pakistan baadaye ilimuachilia Baradar tarehe 21, Septemba, lakini haijulikani aliendа kuishi wapi.

Wakati wa kukamatwa kwake aliidaiwa kuwa naibu wa kiongozi wa kidini wa kundi hilo, Mullah Mohammad Omar, na mmoja ya makomanda aliyemuamini sana.

Viongozi wakuu wa Afghanistan walikuwa na matumaini kwamba mtu kama yeye angeweza kulishawishi kundi la Taliban kufanya mazungumzo na serikali.

Mpango huo wa serikali ulikuwa na malengo ya udhibiti baada ya vikosi vya Nato kuondoka nchini humo 2014.

Baradar ni mmoja wa viongozi wa kundi hilo ambaye amekuwa akipenda kufanyika kwa mazungumzo na Marekani pamoja na serikali iliyoondolewa ya Afghanistan.

### MTHIBITI WA FEDHA

Baada ya kuwa mmoja ya waanzislishi wa kundi la Taliban 1994, Mullah Baradar alijipatia kazi ya kuwa kamanda wa mikakati ya kijeshi.

Alidaiwa kusimamia operesheni za kila siku za kundi hilo na ufadhili kutoka nje.

Alisimamia majukumu muhimu katika vita vyote vikuu nchini Afghanistan, na kusalia kamanda mkuu wa kundi la Taliban katika eneo la magharibi la Herat pamoja na Kabul.Wakati ambapo Taliban walifukuzwa, alikuwa Naibu Waziri wa Ulinzi. Mkewe ni dada yake Mullah Omar.

Kiongozi huyo alikuwa akifanya mashambulizi makali dhidi ya vikosi vya serikali ya Afghanistan.

Mullah Baradar, kama viongozi wengine wa Taliban , analengwa na baraza la usalama la Umoja wa Mataifa , ambalo lilimshirikisha kumwekea vikwazo pamoja na kundi hilo, wamempiga marufuku kusafiri na kuzuia kundi hilo kuuziwa silaha.

Kabla ya kukamatwa kwake 2010, alitoa taarifa kadhaa kwa umma. Lakini mojawapo ya taarifa hizo ilikuwa ya mwaka 2009, mwezi Julai, ambapo alirushiana cheche za maneno la gazeti la Newsweek.

Alipoulizwa kujibu kuhusu kuongezeka kwa idadi ya wanajeshi wa Marekani nchini Afghanistan, alisema kwamba Taliban inataka kuisababishia hasara kubwa Marekani.

Pia alisikika akiapa kuendeleza vita ya Jihad hadi maadui zao watakapoondoka katika ardhi yao.

Kila mara alionekana kumkinga Mullah Omar, kwa kusema alikuwa katika hali nzuri na kuongoza vita dhidi ya muungano wa Marekani, huku akikana madai kwamba viongozi wa Taliban walikuwa wamepiga kambi Pakistan.

Alipoulizwa kuhusu masharti yao ya kuleta amani, alijibu: Masharti ya msingi ni kuondoka kwa vikosi vya kigeni katika ardhi ya Afghanistan.

Kulingana na polisi ya kimataifa interpol , Mullah Baradar alizaliwa katika Kijiji cha Weetmak wilayani Dehrawood katika mkoa wa Uruzgan mwaka 1968.

Lakini pia anatambulika kutoka kwa kabila la Durrani kutoka tawi la Popalzai , sawa na aliyekuwa rais wa zamani wa Afghanistan Hamid Karzai.

Anaripotiwa kuwa alikuwa karibu na ndugu wa rais Karzai , Ahmad Wali Karzai, ambaye ndiye aliyekuwa mkuu wa baraza la mkoa wa Kandahar kutoka 2005 hadi alipouawa mwaka 2011.

### KAMATAKAMATA YAANZA

UMOja wa mataifa umetoa taarifa yake ukidai wanamgambo wa Taliban, wako kwenye operesheni ya kuwatafuta watu waliofanya kazi na vikosi vya Nato na serikali ya zamani ya Afghanistan.

Umesema wapiganaji hao wamekuwa wakienda nyumba kwa nyumba kuwatafuta wanaowalenga na kuzitishia familia zao.

Kundi hilo lenye msimamo mkali wa Kiislamu limejaribu kuwahakikishia usalama Waafghanistan tangu walipotwaa madaraka, na kuahidi hakutakuwa na ulipaji wa kisasi.

Hata hivyo, Lakini kuna dalili kwamba Taliban wamebadilika kidogo tangu walioonyesha ukatili mwaka 1990.

"Kuna idadi kubwa ya watu ambao kwa sasa wanalengwa na Taliban na tishio liko wazi," anasema Christian Nellemann, ambaye anaongoza jopo la walioandaa ripoti hiyo.

"Waliwapa watu maandishi yanayosema wasipojisalimisha, basi Taliban watakawamata na kuwashtaki, na kuwaadhibu wanafamilia kwa niaba ya watu hao." Anaongeza.

Alionya kuwa mtu yeyote kwenye orodha ya Taliban yuko katika hatari kubwa, na kwamba kunaweza kuwa na mauaji ya watu wengi.

**BBC.**

HABARI KIMATAIFA

## Taliban yawarejea viongozi wa dini

**Kabul,** AFGHANISTAN

KUNDI la wanamgambo wa Taliban, limewatolea wito viongozi wa dini ya Kiislamu, Afghanistan kuhimiza amani wakati wa sala ya jana, ambayo ni ya kwanza tangu wapiganaji wake walipochukua udhibiti wa taifa hilo.

Taliban imewataka maimamu kutumia mahubiri ya ibada ya leo kuhimiza watu kulinda amani na utulivu pamoja na kuwashawishi kutoikimbia nchi, baada ya kuongezeka kwa wasiwasi kwamba utawala wa kundi hilo utakuwa wa kikatili.

Wito wa Taliban unakuja wakati maandamano ya kulipinga kundi hilo yakisambaa kwenye miji mingi Afghanistan, ikiwamo mji mkuu, Kabul na kuna ripoti za watu kuuawa.

Mashuhuda walisema watu kadhaa wameuawa baada ya wapiganaji wa Taliban kufyatua risasi za moto kwenye mkusanyiko mkubwa katika mji wa Mashariki wa Asadabad juzi, Alhamisi.

Ingawa kwa jumla Afghanistan imekuwa na hali ya utulivu, kumekuwa na ripoti za wapiganaji wa Taliban kutumia nguvu kuwadhibiti waandamanaji.

**BBC**

## Wanawake kunufaika na dola bilioni 40

**New York,** MAREKANI

MKUU wa Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa (UNWOMEN), anayeondoka mamlakani, Phumzile Mlambo Ngcuka, ana matumaini kuwa katika kipindi cha miaka mitano dola bilioni 40 zilizoahidiwa zitasaidia, kuhamasisha usawa wa jinsia.

Ngcuka amesema fedha hizo zitapelekea wanawake zaidi kuingia kwenye nyadhifa za uongozi, kupunguza manyanyaso dhidi ya wanawake, pamoja na kuinua hali ya kiuchumi ya zaidi ya wanawake milioni 40 waliyotumbukia kwenye umaskini kutokana na janga la corona.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AP, Ngcuka, alijibu mahojiano kabla ya kujiuzulu kama mkuu wa shirika la UN Women, baada ya kuhudumu kwa miaka nane.

Aliongeza kusema kuwa anaamini wahisani kutoka sekta binafsi pamoja na mashirika, wata heshimu ahadi walizotoa wakati wa kongamano la kuzungumzia usawa la Generation Equality Forum, lililomalizika Julai 2, mjini Paris Ufaransa.

Alisema kuwa kikao ni cha kihistoria katika kuangazia masuala tofauti yanayohusu wanawake.

**VOA**

# Uganda yasitisha shughuli za NGO 50

**Kampala,** UGANDA

MAMLAKA nchini Uganda zimesitisha shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) yapatayo 50, kutokana na kukiuka sheria.

Mashirika mengine yamezuiwa kuendelea na shughuli zao kwa muda usiojulikana, kwa kushindwa kujiandikisha na kupata leseni zao na mengine kwa kushindwa kuwasilisha mahesabu yaliyofanyiwa ukaguzi wa mapato ya kila mwaka kwa Ofisi ya Kitaifa ya NGO.

Taarifa iliyotolewa na Ofisi hiyo jana, inasema kwamba mengine yamekuwa yakifanya kazi bila hata kusajiliwa.

Ofisi hiyo, ambayo ni idara ya Wizara ya Mambo ya Ndani, inasimamia usajili na shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali kote nchini.

Mengi ya mashirika hayo hushughulika na haki za binadamu na masuala ya sera ilhali mengine yanafadhiliwa na mashirika ya kidini na yale ya kutetea haki za wanawake.

Wale ambao kazi yao zimesimamishwa kwa muda usiojulikana ni pamoja na Chapter Four Uganda, iliyoanzishwa na kuongozwa na wakili maarufu wa haki za binadamu Nicholas Opiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, shirika hilo halijawasilisha vitabu vyake vya mahesabu tangu 2016.

Opiyo alikamatwa na kufungwa jela Desemba, mwaka jana na kushtakiwa kwa utakatishaji fedha wakati mamlaka ilipochunguza chanzo cha fedha kwa shirika lake.

Baadaye alipewa dhamana lakini bado anakabiliwa na mashtaka.

Opiyo kupitia ujumbe wa twitter alisema watawasilisha ushahidi na risiti za kuthibitisha kwamba wametekeleza sheria zote na kulipia ada zao pamoja na kuwasilisha vitabu vyao vya mahesabu kwa bodi hiyo.

**BBC**



Watu wakivuka mto Ganga katika jimbo la Patrana nchini India ambao umefurika maji kutokana hali mbaya ya hewa inayosababisha kunyesha mvua nyingi **(Picha: FPA)**

# Mcheza soka maarufu afariki Afghanistan akidandia ndege

**Kabul,** AFGHANISTAN

MAMLAKA ya Afghanistan imethibitisha kwamba mwanasoka kijana alifariki dunia baada ya kujaribu kuondoka nchini humo kwa kudandia ndege ya jeshi la Marekani na kuanguka uwanja wa ndege wa Kabul.

Zaki Anwari (19), aliwahi kuichezea timu ya taifa ya vijana, Afghanistan.

Maelezo zaidi ya ni lini alifariki dunia bado hayajawekwa wazi.

Tangu Taliban kuteka nchi ya Afghanistan, maelfu ya watu wamejitokeza kwenye uwanja wa ndege wa Kabul, wakati ambapo nchi za Magharibi zinakimbilia kuhamisha raia wao na wenzao wa Afghanistan.

Picha ziliibuka Jumatatu wiki hii, zikionyesha mamia ya watu wakikimbia kufuata ndege ya jeshi la anga la Marekani wakati ikishuka kwenye barabara ya kupaa.

Watu wengine walionekana wakishikilia upande mmoja wa ndege.

Ripoti za vyombo vya habari vya eneo zinasema kwamba watu wasiopungua wawili waliuawa baada ya ndege hiyo kupaa.

Kikosi cha anga cha Marekani pia kimethibitisha kuwa mabaki ya binadamu yalipatikana katika vifaa vya kutua vya ndege baada ya kuwasili Qatar.

**DW/BBC**

## China yapitisha sheria mpya ruksa kuzaa watoto watatu

**Hongkong,** CHINA

CHINA imefanya marekebisho rasmi kwa sheria zake, ili kuwaruhusu wanandoa kuwa na watoto hadi watatu, ili kuongeza kiwango cha kuzaliana.

Kanuni hiyo ilikuwa moja kati ya kadhaa zilizopitishwa jana kwenye mkutano wa wabunge wa bunge la kitaifa National People Congress (NPC).

Maelezo juu ya sheria yenye utata ya kupambana na vikwazo dhidi ya Hong Kong, ambayo wafanyabiashara wengi walihofia ingewaweka katika wakati mgumu, pia ilitarajiwa kutajwa.

Vyombo vya habari vya Hong Kong viliripoti jana kwamba uamuzi huo umecheleweshwa.

China ilitangaza mwezi Mei, mwaka huu kwamba, itawaruhusu wanandoa kuwa na watoto hadi watatu, katika mabadiliko makubwa ya sera.

Uamuzi huo sasa umepitishwa rasmi kuwa sheria, pamoja na maazimio kadhaa ambayo yalilenga kuongeza kiwango cha kuzaliana na kupunguza mzigo wa kulea mtoto, lilisema shirika la habari la Xinhua.

Hii ni pamoja na kufuta ada ya uendelezaji jamii, adhabu ya kifedha kwa wanandoa hulipwa kwa kuwa na watoto zaidi ya idadi iliyoidhinishwa, kuhimiza serikali za mitaa kutoa likizo ya wazazi, kuongeza haki za ajira za wanawake na kuboresha miundombinu ya utunzaji wa watoto.

Takwimu za hivi karibuni za sensa zilionyesha kupungua kwa kasi ya kiwango cha kuzaliana.

**BBC**

# Serikali yaonya mabalozi kesi ya Freeman Mbowe

Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amekutana kwa mazungumzo na mabalozi, wakuu wa taasisi na mashirika ya kimataifa yaliyopo nchini, kwa lengo la kuwapa mrejesho kuhusu Mkutano wa 41 wa wakuu wa nchi na serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Vilevile, waziri huyo ametoa angalizo kwa mabalozi wanaokwenda mahakamani kufuatilia kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kwamba wanapaswa kufuata taratibu za kisheria zilizowekwa.

Jijini Dar es Salaam jana, Balozi Mulamula alisema wakuu wa nchi na serikali katika mkutano huo uliofanyika Lilongwe, Malawi Agosti 17 -18 mwaka huu, kwa pamoja walikubaliana kuendelea kukabiliana na janga la UVIKO -19 ikiwa ni pamoja na kushawishi kampuni zinazozalisha chanjo kutoa kibali, ili teknolojia yao itumike kuzalisha chanjo hizo katika nchi zinazoendelea kurahisha upatikanaji wa chanjo hiyo kwa wote na kwa bei nafuu.



Pia aliwaeleza mabalozi, wakuu wa taasisi na mashirika kuhusu ombi la wakuu wa nchi na serikali wa SADC kuzisihi taasisi za fedha za kimataifa pamoja na nchi zilizoendelea kutoa msamaha au kurefusha muda wa urejeshwaji wa mikopo hadi pale janga la UVIKO-19 litakapopatiwa ufumbuzi.

Kuhusu ushiriki wa Tanzania katika mpango wa SADC wa kupeleka jeshi katika Jimbo la Cabo Delgado, Msumbiji, Balozi Mulamula alisema suala la ulinzi na usalama kwa nchi za SADC ni ulinzi na usalama kwa Tanzania, hivyo Tanzania imeshiriki kikamilifu kwa kutoa mchango wake wa fedha pamoja na jeshi.

Balozi Mulamula, pia alitoa msisitizo kwa mabalozi wanaokwenda mahakamani kufuatilia mwenendo wa kesi inayomkabili Mbowe, kufuata sheria na taratibu za kimataifa kuhusu masuala ya kidiplomasia, ili kujiepusha na ukiukwaji wa sheria na taratibu hizo.

Balozi Mulamula alifafanua kuwa serikali haina lengo la kuwazuia mabalozi hao kwenda mahakamani kufuatilia kesi hiyo, lakini kutokana na uwapo wa janga la UVIKO-19 pamoja na msongamano, ni muhimu kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kufuatilia shauri hilo kwa njia nyingine ikiwamo kupitia vyombo vya habari.

Alisisitiza wizara yake ndio yenye jukumu la kuhakikisha usalama wa wanadiplomasia waliopo nchini.

Hata hivyo, kwa siku za karibuni baadhi ya wanadiploamasia hao wameonekana mahakamani bila kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia masuala ya kidiplomasia ikiwamo kutoa taarifa kwa wizara hiyo.

Kiongozi wa mabalozi waliopo nchini, Dk. Ahamada El Badaoui, alisema ulinzi wa mabalozi waliopo nchini ni muhimu sana na kuongeza kuwa endapo kuna mabalozi wanafanya hivyo, ni vyema wakafuata taratibu na sheria zilizopo, jambo lililoungwa mkono na Balozi wa Zambia nchini, Benson Keith Chali.

Katika mkutano huo, baadhi ya mabalozi walipongeza mafanikio yaliyopatikana na kueleza kuridhishwa na namna uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan unavyoendesha shughuli zake pamoja na namna unavyotatua kero mbalimbali.

***Imeandaliwa na Beatrice Inyasi, Kalebo Mussa na Tunu Hassan (TURDACo)***

## Ajali ilivyoua watano na kujeruhi wanane

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU watano wamefariki dunia na wengine wanane kujeruhiwa baada ya gari lililokuwa limebeba nguruwe kuacha njia na kupinduka.

Chanzo cha ajali hiyo kimetajwa kuwa ni uwapo wa mteremko wenye kona kali kwenye barabara ya Babati-Kondoa na hakuna alama za tahadhari.

Akithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema ajali hiyo ilitokea jana saa 12 asubuhi katika Kijiji cha Salanka wilayani Kondoa ikihusisha gari hilo aina ya Fuso lenye namba za usajili T428 CPQ lililokuwa linaendeshwa na dereva Joseph Happyson (32) liliacha njia na kupinduka wakati likitokea Mkoa wa Manyara kuelekea Dar es Salaam.

Alisema gari hilo lilikuwa limebeba nguruwe 135 ambapo kati yao 35 wamekufa.

Aliwataja watu waliofariki kuwa ni James Julius, Joshua Paul na wengine watatu bado majina yao hayajafahamika.

Kamanda huyo aliwataja majeruhi wa ajali kuwa ni Paul Mathayo, Nicodem Alfonce, Joseph Happyson, Salehe Juma, Hamadi Aitooi, Nada Haitoo, Guban Bardei na Patrick Yeda.

"Barabara ina kona kali na mara nyingi eneo hili lina ukungu wakati wa alfajiri na hakuna alama inayoonyesha kwamba sasa unafika eneo lenye kona kali.

"Nitoe wito kwa wenzetu wa TANROADS (Wakala wa Barabara) warudishe alama iliyokuwapo ili kujiepusha na ajali," alisema.

Alitoa wito kwa madereva kuelewa eneo hilo lenye milima ya Kolo lina kona kali kulingana na mazingira ya barabara iliyojengwa, hivyo wachukue tahadhari na kuendesha kwa mwendo ambao si mkali.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**WANATAKIWA WAFANYAKAZI 10 WA LAUNDRY** WENYE ELIMU YA KIDATO CHA NNE,ENEO SINZA NA MBEZI BEACH. MAWASILIANO. WHATSAP ONLY: **0757 129 546**
**INSTAGRAM:@dakikalaundry**

**Kwa Habari Motomoto**
**usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAPILI 22/8/2021 kampuni ya LOGISTIC SUB SAHARA** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA kuelekea MTUKULA** gari hilo lenye namba za usajili**: 35 0SSC FS/252 SSC FA**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 22**
   **Upana - mita 4.00**
   **Kimo - mita 4.80**
3. Njia itakayotumika **TUNDUMA** hadi **MTUKULA** ***kupitia MIKUMI gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

116418302

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**BALTAZARY EDWARD MPINA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye namba za usajili **T 564 AMW** chasis namba **P2J750002031** engine namba **IP20004453,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **PWA/KIB/RB/4069/2021**

21647802

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF LANDS HOUSING AND HUMAN SETTLEMENTS DEVELOPMENT**

**Ref.NO.LR/T/MRLR/10251/18**
**JOSEPH STEPHEN SIGORY**
**P.O.BOX 444**
**MUSOMA**

**THE LAND REGISTRATION ACT (CAP. 334)**

**LOSS OF CERTIFICATE OF TITLE NO 10251.**

Refer the heading above and your application for issuance of new certificate of Title dated 23 April, 2021.

According to the application produced, you cannot trace the certificate of Title. This will necessitate the publication of a notice in the official Gazettes under the provisions of section 38 of the above Act. After one month from the date this notice is published in the official Gazettes a copy of which is enclosed herewith and in the absence of any objection. The new certificate of Title will be issued and forwarded to you.

**J. J Songora**
**ASSISTANT REGISTRAR OF TITLES**
**28/04/2021**

21647702

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 105 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU DR.COL.MOSES BEATUS MINLA MWOMBAJI COL.HOJA SIMON NGW'ESHEMI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuhudhuria mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16 mwezi 09 mwaka 2021

**Imewasilishwa dar es salaam leo tarehe 17 mwezi 08 mwaka 2021**

NAIBU MSAJILI

21648402

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Alinikimbia au kunitoroka wiki moja tu baada ya kufunga ndoa. Sijafaidi kabisa raha ya ndoa. Sijajua ni kwa nini amefanya hivi. Nimekuja huku baada ya kupata taarifa za watu mbalimbali, wengine ndiyo wakanileta hadi huku kwenye baa yenu. Wakaniambia huwa anaonekana huku akiwa na mwaname mwingine. Ndiyo maana niliamua kujibadilisha ili nishuhudia. Na kweli nimeshuhudia, japo imeniuma sana." Alisema Tom kwa uchungu, kwa mbali machozi yalianza kumchuruzika

Woga ulikuwa umeshaondoka kabisa kwenye moyo wa Tedi, huruma ikashika nafasi yake.

Akainuka kutoka kwenye kitanda. Akamsogelea taratibu mpenzi wake. Kwanza akambusu. Akamnyanyua kutoka kwenye kiti. Akamkumbatia na kumsogeza kitandani. Alichotaka kufanya ni kumliwaza na kumbembeleza, kama alivyofanyiwa yeye wakati akihadithia madhila yake.

"Pole sana baba. Pole mpenzi wangu." Tedi alimbembeleza, sasa akiwa ameshatambua kuwa Tom hakuwa jini, zimwi, wala jambazi, ila alilazimika ajibadilishe kwa ajili hiyo.

"Hapa nilipo kila kitu nimeshajua kuwa mke wangu ametorokea Morogoro na yupo na mwanaume mwingine."

"Sasa utafanyaje. Nakuomba usilipe kisasi wala kufanya jambo lolote baya."

"Kama ningetaka kufanya chochote kibaya ningekifanya jana pale kwenye baa ya Mwenda na wewe usingejua mimi nimemuua mtu au watu kwa sababu gani. Ningekuwa nimeshaua, nimetoroka au kukakamtwa tu."

"Kumbe una akili sana mpenzi wangu."

"Ninachotaka kujua hapa ni kwamba kwa nini Farida amenifanyia hivi. Si kawaida kwa mwanamke kukubali kuolewa, halafu wiki moja tu baadaye anakutoroka. Halafu anaonekana tena na mwanaume mwingine. Hapa kuna kitu ambacho sikijui ambacho ndiyo nakitafuta."

Tedi alimtazama Tom kwa jicho la huruma. Lakini baadaye ni kama wivu ukaanza kumuingia.

Aliona kama msaada wa ada ambao ameahidiwa na Tom, kama ikitokea akampata mkewe na kurudiana yeye atakuwa hatarini.

Tedi alimuona Tom si moja kati ya wale wanaume wanaowafanya wanawake ni chombo cha kujifurahisha. Alikuwa anataka kumng'ang'ania kwa vyovyote vile awe naye.




**"Ndiyo mimi nahitaji pesa kwa ajili ya kujikimu kimaisha na pia kulipa upatu tunaocheza ili nipate pesa za ada ya kwenda chuo, lakini simkubali kila mwanaume. Na hata hao wanaume wenyewe nafanya hivyo kwa shida tu. Kama ningekuwa na kazi yangu nzuri, au nimetoka katika familia yenye uwezo. Au hata wazazi wangu wangekuwa hai, haya yote yasingenikuta."**

Kwa muda mfupi tu aligundua kuwa ni aina ya wanaume ambao alikuwa anawatafuta.

Wasikivu. Wanyenyekevu. Wanajali na wapo kutoa msaada, wa ziada mbali na ule wa ujira wa kazi husika.

Alimshangaa Farida kumkimbia Tom. "Kweli kwenye miti hakuna wajenzi. Ningempata mimi huyu?" Alijisemea kimoyomoyo.

Hakutaka kumuuliza Tom mipango yake ya baadaye iwapo atafanikiwa kumpata mkewe.

"Sasa utafanyaje?" Akamuuliza.

"Nachotaka nipeleleze, nijue kila kitu kilichofanyika kabla ya kuamua nini nifanye."

"Nimekwambia usilipize kisasi sawa?"

"Hilo najua."

"Kwani mkeo ni mwenyeji wa huku Morogoro?"

"Ndiyo. Amezaliwa huku, kukulia na kusomea huku. Ukubwani ndiyo akaja kwa dada yake Kigamboni. Mimi nilikutana naye Dar es Salaam na nikampenda, ndoa ikafungwa huku Moro, tukarudi Dar kabla ya haya yalivyotokea."

"Yule baba aliyekuwa naye unamfahamu?"

"Hapana. Wewe unamfahamu?"

"Namfahamu kijuujuu tu. Anaitwa Sam."

"Anaishi wapi?"

"Nasikia anaishi Mwembesongo, ila mwenzangu, anapenda wanawake yule baba."

"Wewe ameshawahi kukutongoza?" Tom aliuliza huku akimtazama kwa makini usoni Tedi.

"Ndiyo, lakini nilimkatalia."

Tom aliona kama vile amedanganywa, akaangua kicheko, lakini si halisi.

"Yaani unafanya kazi pale Mwenda baa, halafu mwanaume kama yule anakutaka, ukakataa?"

Tedi alikunja sura. Kwa mara ya kwanza Tom aliona sura iliyokasirika ya msichana yule.

"Sikiliza Tom, sio kwa sababu nimekukubalia wewe ukadhani mimi ni kahaba sana."

"Mimi sijasema wewe ni uko hivyo."

"Ngoja kwanza nimalize ndiyo utasema." Tedi alimkatisha. Kisha akaendelea.

"Ndiyo mimi nahitaji pesa kwa ajili ya kujikimu kimaisha na pia kulipa upatu tunaocheza ili nipate pesa za ada ya kwenda chuo, lakini simkubali kila mwanaume. Na hata hao wanaume wenyewe nafanya hivyo kwa shida tu. Kama ningekuwa na kazi yangu nzuri, au nimetoka katika familia yenye uwezo. Au hata wazazi wangu wangekuwa hai, haya yote yasingenikuta."

"Hapana mpenzi, sikuwa na maana hiyo." Akaomba radhi.

"Mimi yule Sam kwanza anamtongoza kila mwanaumke akimkuta, halafu hivi sasa anakuja na mwanamke yule pale karibuni kila siku, mimi nitamkubali vipi mwanaume wa aina hiyo, asiyepisha chambo?"

Akili ya haraka haraka ikamjia Tom ya kufanya mpango kabambe ya kutelekeza azma yake.

"Unasikia mpenzi wangu Tedi?"

"Nakusikia."

"Naomba uwe msaada wangu katika hili."

"Msaada upi Tom?"

"Huu wa mke wangu na huyo Sam, wanaishi wapi, nini kimetokea hadi hali hii imetokea. Lakini kwa kukutumia wewe."

Tedi alishtuka "Kwa kunitumia mimi?" Akauliza kwa mshangao.

"Ndiyo. Wala si kwa ubaya. Kwa sababu Sam alikutongoza. Nataka umkubalie, halafu kuna vitu nitakutuma ili uvifuatilie na maswali fulani ambayo yanaweza kunifanya nipate mwanga wa hili."

Tedi bado alikuwa kwenye mshangao. "Hivi wewe Tom una wazimu? Yaani unaniruhusu nikatembee na Sam. Tena mtu ambaye anatembea na mkeo? Kwa hiyo atuchanganye wote wawili uone raha ee. Hivi wewe ni mwanaume gani? Mwanaume wa wapi?" Tedi aliongea kwa ukali na hapo akanyanyuka ili avae nguo zake.

Tom alimkamata kwa nguvu. Alimrudisha tena kitandani. Alijua maneno aliyosema ni kama kumdhalilisha. Kumtuma aende kwa mwanaume mwingine ni kumfanya kama ni mwanamke asiye na thamani.

"Tulia Tedi. Naomba tuelewane. Maana yangu siyo hivyo unavyodhani. Usidhani mimi ni mjinga kiasi hicho. Nitachotaka hapa ni msaada tu kwako kwa sababu tayari huyo Sam alikuwa na nia ya wewe. Nachotaka ni kwenda naye. Yeye akiwa na hamu na wewe, lakini unakwenda kwenye kazi maalum. Utakwenda huko nikiwa nimechukua hatua zote zitakazofanya asifanye chochote na wewe. Utakuwa ukifanya kila kitu kwa maelekezo yangu na kama ukiyafuata, hatokufanya chochote. Hatokugusa na wewe utapata ulichokifuata." Tom aliongea kwa msisitizo. Ni sauti ya mamlaka ambayo Tedi hakuwahi kuisikia kabla. Ilimfanya atue tuli.

"Siwezi kukupeleka kwa mwanaume mwingine. Kuanzia leo utakuwa chini yangu hadi hapo nitakapoupata ukweli wote kuhusu mke wangu Farida."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

MECHI KALI
HOME
MANCHESTER CITY
1.15 | 7.62 | 17.78
NORWICH CITY
AWAY

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
halopesa
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 433

# JORGINHO, N'GOLO, BRUYNE WACHUANA TUZO YA UEFA



**LONDON, England**

VIUNGO wa Chelsea, Jorginho na N'Golo Kante pamoja na nyota wa Manchester City, Kevin de Bruyne wameingia kwenye tatu bora ya wachezaji wanaowania tuzo ya Mchezaji Bora wa mwaka wa Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA).

Kwa upande wa tuzo ya kocha bora wa mwaka, walimu wanaowania ni Pep Guardiola wa Manchester City, Thomas Tuchel wa Chelsea na Roberto Mancini wa Timu ya Taifa ya Italia.

Kwa mara ya kwanza tangu tuzo hiyo ianzishwe miaka 11 iliyopita, wachezaji wote wanaume wanaowania tuzo hiyo ni viungo.

Jorginho na Kante walishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa na kocha wao, Tuchel pale Chelsea, wakiwafunga De Bruyne na Guardiola na Manchester City yao kwenye fainali.

Jorginho pia alishinda taji la mataifa ya Ulaya, Euro 2020, pamoja na kocha wake, Mancini.

Kwa upande wa wachezaji wanawake watatu wanaowania tuzo hiyo ni mshindi wa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa wanawake akiwa na Barcelona, Jenni Hermoso, Lieke Martens na Alexia Putellas.

Kocha wa Timu ya Wanawake ya Chelsea, Emma Hayes ameingia kwenye kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya kocha bora wa mwaka, akipambana na wa Barcelona, Lluis Cortes na Peter Gerhardsson wa Sweden.

Hayes aliiongoza timu ya wanawake ya Chelsea kutwaa taji lao la nne la Ligi Kuu kwa kipindi chake cha miaka yake tisa hapo Chelsea na kuifikisha fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya kwa wanawake.

Washindi wa tuzo hiyo watatangazwa kwenye sherehe zitakazofanyika jijini Istanbul nchin Uturuki, Agosti 26, 2021 wakati pia kutafanyika droo ya ratiba ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

# Messi amjaza 'noti' Jordan

**PARIS, Ufaransa**



GWIJI wa mpira wa kikapu wa Marekani, Michael Jordan hadi sasa amepata karibu euro milioni sita kutoka kwenye mauzo ya jezi zote za PSG zilizouzwa na jina la Lionel Messi, kwa mujibu wa Marca.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Jordan anapata asilimia tano kwa jezi yoyote inayouzwa na PSG, kwani mavazi ya klabu hiyo yanadhaminiwa na chapa ya Nike ya Air Jordan.

Kwa hali ilivyo, kuwasili kwa Messi katika mji mkuu wa Ufaransa, Paris, kumeipatia PSG karibu euro milioni 120 kupitia mauzo ya jezi kitu ambacho kinamaanisha Jordan ametia mfukoni karibu euro milioni sita.

Kwa mujibu wa Forbes, nyota huyo wa zamani wa Chicago Bulls alipoteza utajiri wake mwingi kutokana na mlipuko wa janga la virusi vya corona na inadaiwa amepoteza karibu asilimia 24 ya thamani yake ambayo imepungua kutoka dola bilioni 2.1 hadi dola milioni 1.6.

Messi ni mchezaji wa pili anayeuza zaidi baada ya Cristiano Ronaldo na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amejiunga na PSG kwa mkataba wa miaka miwili na chaguo la kuongeza mwaka mwingine.

PSG inaweza kutarajia kuuza jezi nyingi zaidi ya chapa ya Air Jordan katika siku zijazo.

HABARI MICHEZO

# 3,401,140

# JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/08/21 | 17:00 | Crystal Palace vs Brentford | 2.70 | 3.10 | 2.75 |
| 02. 21/08/21 | 17:00 | Leeds vs Everton | 2.22 | 3.53 | 3.12 |
| 03. 21/08/21 | 17:00 | Coventry vs Reading | 2.20 | 3.25 | 3.20 |
| 04. 21/08/21 | 17:00 | Cardiff vs Millwall | 2.24 | 3.21 | 3.16 |
| 05. 21/08/21 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.76 | 3.25 | 2.47 |
| 06. 21/08/21 | 18:00 | Alaves vs Mallorca | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 07. 21/08/21 | 19:30 | Verona vs Sassuolo | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 21/08/21 | 20:30 | Granada vs Valencia | 2.49 | 3.28 | 2.87 |
| 09. 22/08/21 | 16:00 | Wolverhampton vs Tottenham | 3.42 | 3.22 | 2.21 |
| 10. 22/08/21 | 16:00 | Lokomotiv Moscow vs FC Krasnodar | 2.40 | 3.36 | 2.77 |
| 11. 22/08/21 | 16:00 | Bordeaux vs Angers | 2.80 | 3.30 | 2.48 |
| 12. 22/08/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Malaga | 2.73 | 2.78 | 2.87 |
| 13. 22/08/21 | 21:45 | Nice vs Marseille | 2.88 | 3.18 | 2.48 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 21 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2070 | Liverpool vs Burnley | 1.20 | 6.65 | 14.11 |
| 14:30 | 4797 | QPR vs Barnsley | 2.09 | 3.31 | 3.41 |
| 16:00 | 3513 | CSKA Moscow vs Akhmat Grozny | 1.58 | 3.94 | 5.33 |
| 16:00 | 3597 | Arsenal Tula vs Spartak Moscow | 4.64 | 3.70 | 1.70 |
| 16:30 | 2019 | Hertha BSC vs VfL Wolfsburg | 3.03 | 3.42 | 2.26 |
| 16:30 | 2097 | VfL Bochum vs Mainz | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 16:30 | 3452 | Eintracht Frankfurt vs Augsburg | 1.58 | 4.36 | 4.96 |
| 16:30 | 4652 | Greuther Furth vs Arminia Bielefeld | 2.52 | 3.32 | 2.72 |
| 16:30 | 5640 | SC Freiburg vs Borussia Dortmund | 5.19 | 4.50 | 1.54 |
| 17:00 | 1095 | Bournemouth vs Blackpool | 1.62 | 3.69 | 5.31 |
| 17:00 | 1441 | Luton Town vs Birmingham | 2.09 | 3.26 | 3.45 |
| 17:00 | 1918 | Cardiff vs Millwall | 2.32 | 2.96 | 3.26 |
| 17:00 | 2264 | Livingston vs Motherwell | 2.24 | 3.16 | 3.21 |
| 17:00 | 2738 | Derby vs Middlesbrough | 2.77 | 3.01 | 2.62 |
| 17:00 | 2827 | Leeds vs Everton | 2.36 | 3.41 | 2.96 |
| 17:00 | 3192 | Fulham vs Hull City | 1.47 | 4.26 | 6.34 |
| 17:00 | 3222 | Sheffield Utd vs Huddersfield | 1.58 | 3.85 | 5.52 |
| 17:00 | 3359 | Preston vs Peterborough | 2.16 | 3.15 | 3.40 |
| 17:00 | 3742 | Coventry vs Reading | 2.08 | 3.25 | 3.50 |
| 17:00 | 4345 | Blackburn vs West Bromwich | 3.31 | 3.16 | 2.19 |
| 17:00 | 4630 | Stoke City vs Nottingham | 1.85 | 3.35 | 4.23 |
| 17:00 | 5146 | Crystal Palace vs Brentford | 2.56 | 3.17 | 2.86 |
| 17:00 | 5424 | Celtic vs St Mirren | 1.28 | 5.55 | 8.92 |
| 17:00 | 5626 | Manchester City vs Norwich City | 1.15 | 7.62 | 17.78 |
| 17:00 | 5777 | Aston Villa vs Newcastle | 1.82 | 3.82 | 4.12 |
| 18:00 | 1257 | Monaco vs Lens | 1.76 | 3.74 | 4.39 |
| 18:00 | 2202 | Ural Yekaterinburg vs Dinamo Moscow | 4.04 | 3.45 | 1.86 |
| 18:00 | 2467 | Ufa vs Zenit St Petersburg | 6.67 | 4.51 | 1.42 |
| 18:00 | 5397 | Alaves vs Mallorca | 2.28 | 3.17 | 3.33 |
| 19:00 | 3241 | FC Zurich vs Grasshoppers | 1.98 | 3.59 | 3.44 |
| 19:15 | 4868 | Kasimpasa vs Giresunspor | 2.03 | 3.32 | 3.56 |
| 19:30 | 2932 | Bayer Leverkusen vs Monchengladbach | 2.27 | 3.53 | 2.93 |
| 19:30 | 3010 | Brighton vs Watford | 1.71 | 3.57 | 5.24 |
| 19:30 | 4648 | Inter vs Genoa | 1.37 | 5.03 | 8.04 |
| 19:30 | 5291 | Verona vs Sassuolo | 2.56 | 3.46 | 2.66 |
| 19:45 | 2741 | Heerenveen vs Waalwick | 1.75 | 3.66 | 4.35 |
| 20:00 | 3322 | Gil Vicente vs Benfica | 5.31 | 4.04 | 1.56 |
| 20:30 | 4017 | Espanyol vs Villarreal | 3.02 | 3.33 | 2.36 |
| 20:30 | 5499 | Granada vs Valencia | 2.50 | 3.21 | 2.91 |
| 21:00 | 3106 | Sparta Rotterdam vs Heracles Almelo | 2.17 | 3.16 | 3.36 |
| 21:00 | 4128 | PSV Eindhoven vs Cambuur | 1.26 | 5.93 | 9.10 |
| 21:30 | 3225 | St. Gallen vs FC Sion | 1.60 | 4.05 | 4.94 |
| 21:45 | 1492 | Gaziantep BB vs Besiktas | 4.05 | 3.65 | 1.81 |
| 21:45 | 1568 | Alanyaspor vs Altay | 2.03 | 3.20 | 3.70 |
| 21:45 | 4609 | Empoli vs Lazio | 4.54 | 3.93 | 1.72 |
| 21:45 | 5772 | Torino vs Atalanta | 5.21 | 4.31 | 1.58 |
| 22:00 | 1844 | St Etienne vs Lille | 3.04 | 3.19 | 2.37 |
| 22:00 | 1879 | Dinamo Zagreb vs Lokomotiva Zagreb | 1.31 | 4.84 | 8.13 |
| 22:00 | 3440 | Groningen vs Utrecht | 3.55 | 3.65 | 1.92 |
| 23:00 | 3917 | Athletic Bilbao vs Barcelona | 3.87 | 3.53 | 1.95 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# RODRIGUEZ AKANUSHA KWENDA ATLETICO

**MADRID, Hispania**

MAPEMA Jumatatu wiki hii, James Rodriguez alizua uvumi mkali kuwa ana mpango wa kujiunga na Atletico Madrid, wakati akichapisha picha aliyojipiga kwa simu iliyo na kaulimbiu kutoka katika klabu hiyo.

Kwa kuwa alikuwa karibu kujiunga na klabu hiyo miaka miwili iliyopita, ilishangaza wakati anatafuta timu baada ya kubainika wazi hataendelea na Everton.

"Usiache kuamini," aliandika, lakini sasa amekataa uhusiano wowote na Atletico.

"Sikujua kwamba ilikuwa kauli mbiu ya timu hiyo, ilikuwa bahati mbaya kabisa," alisema kwenye Twitter.

"Niliweka tu ujumbe binafsi, sikusema nilikuwa nikienda klabu au mahali popote.

"Imekuwa kwenye habari siku nzima, sijahusishwa na klabu hiyo, hakujakuwa na mazungumzo, hakuna chochote, lakini kila mtu anajua hilo.

"Kama ninakwenda katika klabu sisemi au kutoa ishara, nazungumza inapomalizika kwa sababu chochote kinaweza kutokea kwenye mpira wa miguu.

"Kwa waandishi wa habari na wale ambao huweka vitu kama hivyo, unahitaji kujijulisha vizuri zaidi, sikutaka kuunda ubishani."

Kocha mpya wa Everton, Rafa Benitez ameripotiwa kumwambia hatakuwa na jukumu la kucheza katika klabu ya Merseyside chini ya usimamizi wake.

# Lukaku kuvaa jezi namba 9




**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI mpya wa Chelsea, Romelu Lukaku amethibitisha kuwa, atakuwa anavaa jezi namba tisa baada ya kuondoka kwa Tammy Abraham aliyejiunga na klabu ya AS Roma ya Italia.

Mwanzoni mshambuliaji huyo alipewa jezi namba 18 aliporejea Stamford Bridge kutoka Inter Milan wiki iliyopita, lakini sasa amechukua namba ya Abraham.

Lukaku mwenye umri wa miaka 28 anatarajiwa kuwapo katika mchezo dhidi ya Arsenal kesho Jumapili, ikiwa ni ya kwanza tangu arejee katika klabu ya Chelsea, pia amefanya mazoezi kamili na kikosi chini ya kocha, Thomas Tuchel.

"Je! Ninaweza kusema? Ndio, nina namba 9. Nina furaha na bahati kuwa katika hali hii," alisema katika mkutano na waandishi wa habari.

Raia huyo wa Ubelgiji aliongezea juu ya changamoto ya kuikabili Arsenal katika mchezo wake wa kwanza huko Chelsea: "Wanajijenga na mwisho wa siku, ninaangalia tu timu yangu na kuzingatia kile tulicho nacho.

"Utakuwa mchezo mgumu, lakini tutajiandaa kwa vita."

Alipoulizwa ikiwa yuko tayari kuanza dhidi ya Washika bunduki, Lukaku alijibu: "Nimekuwa nikifanya mazoezi. Nilifanya mazoezi kamili kabla ya msimu.

"Sasa ninajaribu kuboresha wachezaji wenzangu na ninapatikana ikiwa kocha anataka nicheze."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI AOMBA KUONDOKA BAYERN

Lengo lake ni kupata changamoto mpya katika klabu nyingine kabla 'jua' ...

**MUNICH, UJERUMAN**

ROBERT Lewandowski ameomba kuondoka Bayern Munich, ili kwenda kutafuta changamoto mpya, lakini klabu hiyo inataka dau la pauni milioni 100, kwa ajili ya kumwachia, Sky Sport imeandika.

Ikumbukwe Lewandowski alitua Bayern Munich kwa uhamisho huru kutoka Borussia Dortmund, lakini sasa thamani yake ni zaidi ya pauni milioni 100.

Sky Sports imeripoti kuwa Lewandowski, ambaye atatimiza miaka 33 leo Jumamosi, anafuraha Bayern, lakini anataka kupata uhamisho kwa klabu nyingine ya Ulaya kabla ya umri wa miaka 35.

Mabingwa wa Ujerumani, wamepanga kumuweka hadi mwisho wa mkataba wake unaomalizika mwaka 2023.

Anachukuliwa kama mmoja wa washambuliaji bora katika mpira wa miguu ulimwenguni, alifunga mabao 56 kwa klabu na nchi msimu uliopita.

Tayari ameshafunga mabao matatu katika mechi mbili za ushindi za Bayern, pamoja na ushindi wa katikati mwa wiki wa Kombe la Super dhidi ya Borussia Dortmund.

Lewandowski anajulikana sana katika mchezo huo kwa kujitolea kwa hali yake ya mwili, na bosi wa Manchester City, Pep Guardiola aliwahi kumwelezea kama "mchezaji mtaalamu zaidi niliyewahi kukutana naye."

## ZISIKUPITE

### LINGARD NJIA MOJA
KIUNGO wa kati wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, yuko tayari kuondoka Manchester United kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa, isipokuwa kama tu atakuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara kwa timu hiyo ya Kocha, Ole Gunnar Solskjaer msimu huu. ***(Times)***

### LEWANDOWSKI SOKONI
MSHAMBULIAJI wa Poland, Robert Lewandowski yuko tayari kutafuta changamoto mpya mbali na Bayern Munich. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, bado amesalia na miaka miwili kumaliza mkataba wake na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga. ***(Mirror)***

### TCHOUAMENI ANUKIA CHELSEA
CHELSEA imeripotiwa kufanya mazungumzo mapya na kiungo wa kati wa Monaco, Aurelien Tchouameni. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 21, pia amehusishwa na Manchester United katika kipindi chote cha msimu huu. ***(Simon Phillips, via Express)***

### SALAH MAMBO SAFI
LIVERPOOL wanaandaa ofa ya mkataba mpya kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, ambayo itakuwa ghali zaidi katika historia ya kilabu hiyo. ***(Athletic)***

### AUBAMEYANG HAONDOKI
PIERRE-Emerick Aubameyang anafurahi kusalia Arsenal hata baada ya kipindi cha uhamisho. Barcelona ilisemekana kuwa na nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Gabon, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 32 anataka kutimiza lengo lake la kuwa gwiji wa washikabunduki hao. ***(Express)***

### BRIGHTON YAJIPANGA
KLABU ya Brighton ipo kwenye mazungumzo na Benfica juu ya uhamisho wa pauni milioni 25 kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

### DIALLO KITAELEWEKA
KLABU ya Sheffield United inavutiwa kumsajili winga wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 19 kwa mkopo. ***(Sky Sports)***

### VLAHOVIC HAUZWI
RAIS wa Fiorentina, Rocco Commisso anasisitiza kuwa hajaweka bei ya mchezaji wake, anayewaniwa na Manchester City na Tottenham Hotspur, Dusan Vlahovic (21). Mshambuliaji huyo pia amewavutia mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, Atletico Madrid. ***(TGR Rai Toscana, via Inside Futbol)***

### LIVERPOOL NA SARR
KLABU ya Watford hawajapata ofa yoyote kwa winga wake raia wa Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 23, msimu huu na amesalia kuwa mchezaji imara - ambaye amehusishwa na kuhamia Liverpool, lakini hauzwi. ***(Watford Observer)***

### MBAPPE NI MTULIVU
KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino amesema mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ni "mtulivu" tu licha ya uvumi mpya unaomhusisha kuhamia Real Madrid. ***(Metro)***

### SMALL ANUKIA SOUTHAMPTON
KLABU ya Southampton inafikiria kumchukua beki wa Everton, Thierry Small. Kijana huyo mwenye umri wa miaka 17 anahusishwa na kuondoka kule Goodison Park wakati kuna ripoti amekataa kutia saini mkataba mpya na Toffees hao. ***(Hampshire Live)***

**HABARI MICHEZO**

## Tinocco atua Geita Gold FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Geita Gold imetangaza kumsajili aliyekuwa golikipa wa Yanga na Kagera Sugar, Benedict Tinocco pamoja na mshambuliaji, George Mpole, kutoka Polisi Tanzania.

Klabu hiyo ambayo kwa mara ya kwanza itaanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2021/22, tayari imewatambulisha rasmi wachezaji hao.

"Geita Gold FC tunayo furaha kuwaarifu kuwa tumeingia mkataba wa mwaka mmoja na golikipa, Benedict Tinocco 'Buffon', tuliyemsajili kutoka Kagera Sugar. Tinocco ni mmoja wa makipa hodari, aliyewahi kuzitumikia klabu mbalimbali kubwa hapa nchini, ikiwamo Mtibwa Sugar, amekuja kuongeza nguvu kwenye eneo la lango la timu yetu." Iliandika taarifa ya klabu hiyo.

Geita Gold ilisema pia mshambuliaji wao mpya, Mpole amesaini mkataba wa mwaka mmoja.

"Mpole ni miongoni mwa washambuliaji wazuri akiwa ameshatumikia klabu za Majimaji, Mbeya City na Polisi Tanzania. Huo unakuwa ni usajili wetu wa saba kuelekea msimu ujao, tukiwa na nia ya dhati kabisa kufanya vyema kwenye Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la FA," iliongeza taarifa Geita Gold.

## TFF yatambulisha ligi zake kivingine

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limetangaza kubadili majina ya ligi zake mbili kuanzia msimu wa 2021/22 ambapo iliyokuwa Ligi Daraja la Kwanza sasa itajulikana kama Championship.

Ligi nyingine iliyobadilishwa jina ni Ligi Daraja la Pili ambayo sasa itaitwa First League na uamuzi huo umepitishwa na kikao cha Kamati ya Utendaji kilichofanyika hivi karibuni ili kuzipa ubora.

Mkurugenzi wa Sheria na Masoko wa TFF, Boniface Wambura, alisema Championship sasa itachezwa kwa mtindo wa ligi badala ya mfumo wa makundi kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Alisema katika kuhakikisha ligi hiyo inapiga hatua zaidi, kumefanyika maboresho mbalimbali ambayo yatakuwa na tija kwa afya ya mpira wa Tanzania.

"Kwa hapa kilichoangaliwa zaidi ni katika eneo la masoko kuzifanya ligi ziwe na mvuto na kuzipa thamani zaidi na hata kuvutia wadhamini wengi zaidi," alisema Wambura

Alizitaja timu zitakazoshiriki Championship kwa msimu ujao ni pamoja na Ihefu SC, Mwadui FC, JKT Tanzania, Pan African, DTB, Green Warriors, African Sports, Mashujaa, Ken Gold, Transit Camp, Kitayose, Pamba, Fountain Gate, Ndanda FC na African Lyon.

# MENEJA AFUNGUKA WAZIRI KUNUNUA MKATABA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

MENEJA wa straika Waziri Junior, Ismail Mwakabanga, amesema sababu za mchezaji wake kununua mkataba uliobaki wa mwaka mmoja na Yanga ni kutaka kuondoka kwenye klabu hiyo na kwenda sehemu ambayo atapata namba ya kucheza.

Mwakabanga amesema hayo, baada ya taarifa zilizotoka juzi kuwa mchezaji huyo ameachana na Yanga na sasa yupo huru kusajiliwa na klabu yoyote ile.

Meneja huyo alisema anaamini straika huyo sasa atapata klabu ambayo itampa nafasi ya kucheza na kulinda kipaji chake.

Alisema Waziri hajaachwa Yanga kama baadhi ya watu wanavyodai, ila alinunua mkataba wa mwaka mmoja uliobaki baada ya kuona nafasi yake ya kuendelea kucheza kwenye klabu hiyo ni ndogo, hasa baada ya kusajili wachezaji wengine wapya wa ndani na nje ya nchi.

"Kwanza kabisa alikuwa hapati nafasi ya kucheza. Halafu kwa sasa wamesajiliwa mastraika wengine, kwa hiyo tumeona itakuwa ngumu sana kwake kuendelea kupata nafasi, na ni mbaya sana kwa mchezaji yoyote yule kukaa bila kucheza, tukaona ni bora tuununue mkataba uliobaki na kweli klabu ikakubali, sasa yupo huru na hii tumefanya kwa ajili ya kulinda kipaji chake," alisema meneja huyo.

Aliongeza kwa sasa mteja wake yuko huru na ameshapokea maombi kutoka kwenye klabu mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania zinazohitaji huduma yake.

"Hapa ndani kuna klabu kama tatu zinamhitaji, lakini hata nje ya nchi. Nadhani kwa sasa sitoweza kuzitaja timu hizo, nipe muda baada ya siku kadhaa kila kitu kitakuwa wazi," alisema Mwakabanga.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema ni kweli Waziri ameununua mkataba wake na wameshakubaliana kila kitu na kwa sasa yupo huru.

Bumbuli alisema awali walitaka kumuuza na klabu mbalimbali zilikwenda kutaka kumsajili, lakini ofa yao ilikuwa ndogo.

"Kuna klabu zilikuja kutaka kumsajili, lakini ofa yao ilikuwa ndogo tukataa, baadaye yeye mwenyewe akaamua kuununua na hivyo tumekubaliana.

Mchezaji huyo amekuwa na msimu mbaya kwenye klabu hiyo kutokana na kukosa nafasi ya kutosha ya kucheza kama alivyokuwa katika klabu yake ya mwisho ya Mbao FC ya jijini Mwanza.

Yanga ilimsajili mchezaji huyo msimu uliopita akitokea Mbao FC, huku pia amewahi kuzichezea klabu za Toto African na Azam FC



Mshambuliaji wa African Sports inayoshiriki Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza, Ayoub Mbaruku (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Dar City, Salum Mkana katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume Ilala jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam, Biashara United mtegoni CAF*

**Na Saada Akida**

TIMU za Azam FC na Biashara United, zitakazoiwakilisha Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho, zimeanza kuchukua hatua ya kuandaa timu za wanawake ili kukidhi kanuni za Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Hata hivyo kanuni hiyo itaanza kutumika katika msimu wa 2022/23.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema taarifa hizo hazijawafikia rasmi lakini wataanza mchakato huo mapema kwa sababu ndoto zao ni kuendelea kushiriki michuano ya kimataifa.

Popat alisema ameziona taarifa hizo na klabu yake itaanza mchakato huo kwa sura mbili, moja kuanzisha timu yao kuanzia chini au kuinunua timu ambayo itakuwa tayari kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Naye Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso alisema klabu yake imeanza kuzifanyia kazi kwa kujiandaa kisaikoloji mapema huku wakisubiri taarifa rasmi kutoka katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

"Tunatambua hili suala ni mapema kulizungumzia kwa sababu hatujapata taarifa zaidi ya kuona katika mitandao, hatuwezi kudharau zaidi ya kujiandaa kisaikolojia kwa kuangalia nini cha kufanya endapo tutapata taarifa rasmi," alisema Mataso.

Michezo
Jumamosi Agosti 21, 2021
Nipashe



Lewandowski aomba kuondoka Bayern UKURASA 22



Winga mpya wa kimataifa wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kutoka Malawi, Peter Banda (kulia), akimiliki mpira dhidi ya golikipa namba tatu, Ally Salim katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea katika Jiji la Rabat nchini Morocco. **PICHA: SIMBA SC**

# GOMES ATAMBA SIMBA NI MOTO

●●● Yajipanga kufanya vyema na kupata mafanikio zaidi ya waliyopata msimu...

**Na Tunu Hassan, TUDARco**

MAMBO ni moto! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes baada ya kukutana na kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

Simba ni mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu minne mfululizo na mabingwa wa mashindano ya Kombe la FA, kwa misimu miwili mfululizo.

Kikosi hicho cha Gomes kinatarajia kucheza mechi yake ya kwanza ya kirafiki ya kimaraifa leo dhidi ya wenyeji FAR Rabat, inayofundishwa na kocha wa zamani wa Simba Mbelgiji, Sven Vandenbroeck.

Akizungumza na gazeti hili jijini Rabat, Gomes alisema anaridhishwa na kiwango cha kila mchezaji na anafurahi kuona wote wako tayari kutimiza malengo ya klabu hiyo kuelekea msimu mpya wa 2021/22 ambao kwa hapa nchini utaanza rasmi ifikapo Septemba 25, mwaka huu.

Gomes alisema wachezaji wamekuwa wakionyesha ushindani mazoezini na hiyo inampa 'picha' kwamba kila mmoja anahitaji kupata namba kwenye kikosi cha kwanza au kuwa sehemu ya wachezaji 18 ambao wako kwenye mipango ya benchi la ufundi.

Kocha huyo alisema anahitaji kuona wanafanya vizuri zaidi ya mafanikio waliyopata msimu uliopita katika mashindano yote watakayoshiriki na kuifanya bendera ya klabu hiyo kupeperushwa vyema.

"Nimepata nafasi nzuri ya kuwaona wachezaji wote, ni wachezaji wazuri, wanaoonyesha bidii, naridhishwa na namna wanavyojituma," alisema Gomes.

Mfaransa huyo alisema wachezaji wake wamekuwa wakiimarika kadri siku zinavyokwenda na wanaonyesha wana 'kiu' ya mafanikio ya timu na binafsi kwa kila mchezaji.

"Wamekuwa wakijituma sana, unaona kila mmoja anahitaji kuonyesha kitu, hili ni jambo zuri, kwa kifupi niseme kikosi changu kinaimarika zaidi," Gomes alisema.

Aliongeza anashukuru uongozi umesajili wachezaji wapya wa ndani na nje ya nchi kwa kufuata mapendekezo aliyowasilisha na hii imeongeza nguvu ya kikosi chake.

"Tumejiandaa kukutana na ushindani katika kila mechi tutakayocheza, ni lazima tuwe imara na tayari kukabiliana na hali hiyo, changamoto ni jambo la kawaida na kama mwalimu natakiwa niwe tayari kupambana, ingawa nakiona kikosi changu ni bora," alisema Gomes.

Alisema pia amepata nafasi ya kuwapa 'darasa' wachezaji wapya wa timu hiyo ili wafahamu ni klabu ya aina gani ambayo imewasajili, malengo yake na matarajio ya mashabiki.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanafurahia mazingira ya kambi waliyopo.

"Hakuna changamoto yoyote, kila kitu kinakwenda vizuri, programu za mwalimu zinatekelezeka vyema na kila mmoja wetu anafikiria mafanikio tu, tunasubiri muda wa kazi," Rweyemamu alisema.

Simba itaanza msimu mpya kwa kuwavaa watani zao, Yanga katika mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Septemba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam lakini itaanzia hatua ya pili katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Vigogo hao kutoka Mtaa wa Msimbazi Kariakoo jijini wataanza kampeni ya kuwania taji hilo la Afrika dhidi ya Jwaneng

## Yanga yaandaa makubwa 2021

**Na Saada Akida**

KUELEKEA kilele cha Wiki ya Wananchi, uongozi wa Yanga umesema wameandaa 'suprise nyingi' zenye lengo la kuweka rekodi mpya tofauti na ilivyokuwa katika msimu uliopita ambapo walitambulisha wachezaji na benchi la ufundi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa, Suma Mwaitenda alisema kumalizika kwa msimu uliopita ni mwanzo wa msimu mpya ambapo katika kilele cha sherehe hizo, wanatarajia kufanya shughuli mbalimbali za kijamii pamoja na uzinduzi wa jezi mpya.

Mwaitenda alisema kilele cha Wiki ya Wananchi kitakuwa ni Agosti 29, mwaka huu wakati uzinduzi utafanyika kesho Jumapili huko Zanzibar na mgeni rasmi ni Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman.

"Lengo la Wiki ya Wananchi ni kurudisha shukrani zetu kwa mashabiki kwa kufanya mambo mbalimbali ikiwamo kuchangia damu, kupanda miti na kutoa msaada kwa wasiojiweza, tutafungua matawi mawili pamoja na kugawa magodoro katika Hospitali mbili za Mwembeladu na Mnazi Mmoja," alisema Mwaikenda.

Alisema pia kutakuwa na maandamano yatakayoanzia Makao Makuu ya Yanga, kabla ya kuanza maandamano hayo wataenda kumtembelea mlezi wao, Mama Fatma Karume na baadae wataelekea Kisiwa Ndui ambapo 'amelala' Mzee Karume kwa ajili ya kufanya dua.

"Msimu huu tumekuja kivingine kabisa, siku ya kilele kuna mambo mengi ya kuwashtukiza wanachama na mashabiki wa Yanga, ikiwamo kutambulisha baadhi ya watu wa benchi la ufundi pamoja na kauli mbiu yetu ya msimu huu," kiongozi huyo alisema.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema hii ni shughuli yao wananchi na wanapaswa kujitoa na kamwe hawapaswi kuuangusha uongozi.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042